# Nipashe

Jumamosi Novemba 14, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580399

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper LIKE & FOLLOW US





UKURASA 11

**Kumekucha** Baraza la Mawaziri, Prof. Kabudi, Mpango watangulia

UKURASA 2



**Jela** miaka 12 kumkata kidole muuza baa

UKURASA 3

# Mambo msingi hotuba ya JPM

• **Aapa** kupambana na wala rushwa, wanaohatarisha amani, kukuza uchumi kwa asilimia 8, sekta za kipaumbele zatajwa... *Endelea ukurasa 4*



Rais Dk. John Magufuli, akihutubia na kulifungua Bunge la 12, jijini Dodoma jana. Kulia ni Spika wa Bunge, Job Ndugai na kushoto ni Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan. **Picha zaidi Uk. 7. PICHA: BUNGE**

## Asilimia 61 Bunge la 12 ni sura mpya

UKURASA 2

## Gwajima aanza na vijembe Bungeni

UKURASA 2




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

GET IT ON Google Play · Download on the App Store



**MICHEZO** **SIMBA, YANGA HADITHI ILE ILE** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

# JPM aanzia kwa Mpango, Kabudi

**Na Nelson Simon**

BAADA ya kumrudisha Kassim Majaliwa katika nafasi ya Waziri Mkuu wa Tanzania, Rais John Magufuli ameanza kujaza Baraza lake la Mawaziri, akiteua mawaziri wawili.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana saa 10:40 alfajiri na Kurugenzi ya Mawasiliano Ofisi ya Rais, Ikulu, Rais Magufuli amemteua Profesa Palamagamba Kabudi kuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Rais Magufuli pia amemteua Dk. Philip Mpango kuwa Waziri wa Fedha na Mipango.

Mawaziri wateule hao walikuwa wakishikilia nyadhifa hizo katika Baraza la Mawaziri lililopita.

Taarifa hiyo ya Ikulu ilibainisha kuwa uteuzi wa wawili hao ulianza rasmi jana Novemba 13.

Dk. Mpango alikuwa Waziri wa Fedha na Mipango kwa kipindi chote cha miaka mitano ya baraza lililopita wakati Profesa Kabudi aliingia katikati ya safari akiteuliwa kuwa Waziri wa Katiba na Sheria na baadaye kuhamishiwa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, ambayo amerejeshwa tena.

# Sura mpya zatawala Bunge la 12

**Na Waandishi Wetu**

SPIKA wa Bunge, Job Ndugai amesema wabunge ambao wameshaapishwa mpaka sasa ni 359 huku wapya wakiwa 206 sawa na asilimia 61.1.

Sambamba na hilo, Bunge limeahirishwa hadi Februari 2, mwakani huku akisema maspika wastaafu wataanza kuwafunda wabunge wiki ijayo kuhusu wajibu wao.

Ndugai alisema hayo jana bungeni alipokuwa akitoa taarifa ya Spika kabla ya Rais John Magufuli kuhutubia bunge kwa ajili ya kulizindua Bunge la 12 huku akibainisha kwamba kikatiba wabunge wanapaswa kuwa 393 lakini waliopo ni 359.

"Bado tunasubiri wabunge watano kutoka Baraza la Wawakilishi, tunasubiri wateule wa Rais 10 wanawake watano na wanaume watano. Lakini pia tunasubiri viti maalum kutoka vyama vingine kwa kadri watakavyokuwa, hivyo itakuwa 393, 'full house'," alisema.

Alifafanua kuwa kati ya hao 359 kuna Mwanasheria Mkuu wa Serikali, wabunge wa CUF watatu, pia kunapaswa kuwa na wabunge kutoka ACT Wazalendo wanne, Mbunge wa Chadema mmoja na wabunge wa CCM 256.


"Kati ya wabunge hawa wa CCM, viti maalum ni 94 lakini kuna 24 wa majimbo jumla ni 118. Uwakilishi wa kinamama ni mkubwa na Tanzania ni moja ya nchi chache zenye wabunge wengi kiasi hiki kwa kinamama katika Ukanda wetu wa Afrika," alisema.

"Hii inatoa picha mabadiliko kwa wakati mmoja wa miaka mitano huwa ni makubwa sana. Hadi sasa ni asilimia 61.1 wapya, inatoa picha kwamba kukaa hapa ni shughuli. Kuendelea kuwapo hapa si masihara. inabidi mumsikilize Rais na kuzingatia yale atakayoyaeleza hapa unaweza kurudi," alisema.

Katika ufunguzi wa bunge hilo, Viongozi mbalimbali walihudhuria wakiwamo Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, Spika wa Baraza la Wawakilishi, Marais wastaafu Ali Hassan Mwinyi na Jakaya Kikwete, Mawaziri Wakuu wastaafu, Makamu wa Rais wastaafu na Mabalozi.

Wengine ni Wakuu wa Taasisi, Viongozi wa vyama vya siasa, na watendaji mbalimbali wa serikali.

**■Imeandaliwa na Augusta Njoji na Romana Mallya (DODOMA).**



Rais Dk. John Magufuli na Rais mstaafu wa Awamu ya Pili, Alhaji Ali Hassani Mwinyi, wakimsikiliza Rais mstaafu wa Awamu ya Nne, Dk. Jakaya Kikwete, katika viwanja vya Bunge, jijini Dodoma jana, baada ya uzinduzi wa Bunge la 12. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Gwajima aanzisha vijembe, avunja mbavu wabunge

**Na Waandishi Wetu**

MBUNGE wa Kawe, Askofu Josephat Gwajima (CCM), jana aliamsha shangwe bungeni alipoielezea hotuba ya Rais Dk. John Magufuli ya kufungua Bunge la 12.

Akizungumza kwa niaba ya wabunge bungeni jijini hapa, Askofu Gwajima alisema hotuba ya Rais Magufuli kwa akili ya kawaida ya mwanadamu haiwezi kubeba kama haijapata ufunuo kutoka kwa Mungu.

Alisema hotuba aliyoitoa hakuna beberu atakayeipenda kwa mwelekeo aliouonyesha kwa Tanzania.

Akinukuu maneno yaliyowahi kutolewa na Waziri Mkuu wa zamani wa Uingereza, Wiston Churchill, Askofu Gwajima alitamka: "Ukiwa unasafiri halafu ukawa unasimama kila mahali kumtupia mawe kila mbwa anayebweka, hutafika safari yako".

"Mheshimiwa Rais, acha mbwa wabweke tuendelee na safari yetu ya kutekeleza ilani yenye kurasa 303... waziri huyo wa zamani pia aliendelea kusema 'waache wabweke kwa raha zao, lakini wewe kaza mwendo',"Askofu Gwajima alinukuu.

Alisema kitendo cha nchi kujigharamia kwenye uchaguzi na kuachana na fedha zenye masharti, kimeishangaza dunia na mabeberu wameachwa midomo wazi.

"Rais wewe ni mwafrika, umetufanya sisi waafrika dunia yote isione aibu kusema Rais wetu ni John Magufuli, sisi wabunge tulioingia bungeni kwa mara ya kwanza pamoja na wengine wa muda mrefu, tunakushukuru Rais kwa kuwa 'performance' (utendaji) yako ya miaka mitano iliyopita, imewabeba wabunge.

"Bila shaka tumepata kura kupitia wewe, ulikuwa ndiyo tofali la ushindi wetu, kuna maeneo hatukuhitaji kupiga kura, ilikuwa inahitaji kutaja jina lako tu na kura zinakuja, asante sana Mheshimiwa Rais," alisifu.

Askofu Gwajima pia aliishukuru Halmashauri Kuu ya CCM Taifa kwa kuwapitisha wabunge wote aliowaita majabali.

"Mheshimiwa Rais, wabunge wako wote ni majabali, hakuna mnyonge hata mmoja hapa, na kwa namna hiyo, umejipa urahisi sana wa kutengeneza serikali yako, hauhitaji 'vetting' kubwa sana.

"Chukua yeyote, umewapeleka likizo isiyo na malipo watu wa 'vetting' kwa sababu kutoka kaskazini hadi kusini, mashariki hadi huko wabunge wote wanafaa kuitumikia serikali yako," alisema.

Alimshukuru Rais Magufuli kwa kuwapa heshima wabunge wapya na ushindi wake wa kimbunga unaonyesha kesho yake inang'ara kuliko jana.

"Niseme maneno machache kwamba tufani imekoma katika nchi, sasa ni majira mapya," Askofu Gwajima alisema huku akishangiliwa na wabunge wenzake.

Vilevile, alimpongeza Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, kwa ushindi alioupata katika Uchaguzi Mkuu uliofanyika Oktoba 28, mwaka huu.

"Ninakupongeza kaka yangu, Rais wa Zanzibar kwa jinsi ulivyowageuza kichwa chini miguu juu wapinzani Zanzibar na kutudhihirishia kwamba wewe ni nguli na ni jabali, hakika siyo tu daktari wa watu, bali ni daktari wa siasa pia," alisifu.

Spika wa Bunge, Job Ndugai, alisema hotuba ya Rais inaonyesha maono yake na inatia moyo kwa Watanzania.

"Mheshimiwa Rais, nikwambie kwamba Bunge hili la 12 limesheheni watu wa kila aina, nikushukuru Rais, tuna deni kwako na kwa nchi yetu.

"Ulipita ukisema nileteeni huyu, wengine tulikuwa hatuchaguliki kabisa kama Rais asingesema nileteeni fulani. Kwa hiyo, tuna deni tumedhaminiwa kwa wananchi," alisema.

Alisema ni lazima kazi ifanyike vizuri ili wananchi waone sababu ya Rais kutaka wananchi wamletee mtu fulani.

"Tutafanya kazi iliyotukuka kabisa, tutakuwa 'very objective', itakuwa ni hoja na zitachambuliwa kwa umakini kwa faida ya nchi yetu tukiongozwa na hotuba yako bila kumwonea mtu," alisema.

Spika Ndugai alisema mawaziri watakaopata nafasi wajipange ipasavyo maana hakuna kubebana kwa kuwa wanalenga kutekeleza maono aliyo nayo Rais.

**■ Imeandaliwa na Augusta Njoji na Romana Mallya (DODOMA).**

HABARI KITAIFA

# Mbaroni tuhuma kutapeli wakulima

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

JESHI la Polisi mkoani Ruvuma limemkamata mfanyabiashara wa mahindi, Christopher Njako (30), maarufu kwa jina la Bilionea wa Mkako, mkazi wa Kijiji cha Mkako wilayani Mbinga, kwa tuhuma za ujipatia mali kwa njia za udanganyifu.

Njako pia anatuhumiwa kujipatia Sh. bilioni 1.3 kwa njia ya udanganyifu pamoja na utakatishaji fedha.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Ruvuma, Kamishna Msaidizi (ACP) Simon Maigwa, alisema jana kuwa mfanyabiashara huyo alikamatwa juzi na jana alitarajiwa kufikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Ruvuma kujibu mashtaka yanayomkabili.

Alisema Agosti, mwaka huu, Njako alikuwa akinunua mahindi kwa Sh. 75,000 kwa gunia na kuyauza kwa Sh. 45000 kitendo kilichowavutia wakulima wengi na wafanyabiashara kutoka mikoa mbalimbali nchini ambao walifika Mkako kwa lengo la kuyauza mahindi yao na wengine kuyanunua ili kuyapeleka mikoa ya kaskazini na nje ya mchi.

Maigwa alisema ilipofika mwanzoni mwa Oktoba, mwaka huu, biashara hiyo ilianza kuleta dosari, shaka na taharuki kubwa kwa wakulima na wafanyabiashara waliokuwa wamepeleka mahindi yao kuyauza kwake.

Alisema wafanyabiashara na wakulima walimlalamikia Njako kushindwa kuwalipa fedha kutokana na mahindi waliyopeleka kuyauza kwake na wengine kudai kuwa walimpatia fedha ili awapatie mahindi bila mafanikio.

Kamanda Maigwa alisema baada ya kupokea malalamiko hayo, polisi walichukua hatua ikiwamo kufanya uchunguzi wa kina na kuupata ukweli kuwa mfanyabiashara huyo alikuwa akifanya biashara kwa njia ya unjaujanja na kuwatapeli zaidi ya wakulima na wafanyabiashara 1,200 ambao wanadai zaidi ya Sh. bilioni 1.3.

Alisema uchunguzi umebaini Njako amekuwa akitumia fedha hizo kuanzisha miradi mingine binafsi na kwamba amejenga ghala la kuhifadhia mahindi, nyumba ya kulala wageni, nyumba ya kuishi na kununua magari ya kifahari.

Polisi baada ya kujiridhisha katika uchunguzi wake, walimtia mbaroni mfanyabiashara huyo na kumfungulia jalada kwa mashtaka matatu ambayo atafikishwa nayo mahakamani.

# Jela miaka 12, faini mil 2/- kumkata kidole muuza baa

**Na Samson Chacha,** TARIME

MKAZI wa Kijiji cha Kibuyi, Rorya mkoani Mara, Ikonga Chacha, amehukumiwa kifungo cha miaka 12 jela baada ya kupatikana na hatia ya kumkata kidole Tatu Iddi aliyekuwa akimdai Sh. 23,000.

Chacha alikuwa akimdai Iddi fedha hizo kutokana na deni la pombe alizokuwa amekunywa kwenye duka lake la pombe (grocery) na baada ya kumdai kwa muda, alimvamia na kutaka kumkata kichwani kwa panga lakini alipokinga mkono, alimkata kidole na kudondoka chini.

Katika hukumu ya kesi namba 59/2019 iliyosomwa juzi na Jaji John Kahozya wa Mahakama Kuu Kanda ya Musoma, ilielezwa kuwa upande wa Jamhuri umetoa ushahidi ambao umeifanya mahakama kufikia uamuzi huo.

Awali, Wakili wa Serikali, Nimrod Byamungu, alidai kuwa Septemba 12, mwaka jana katika mwalo wa wavuvi wa samaki Kijiji cha Kibuyi, Chacha alimvamia na kumjeruhi kwa panga Idd na kumkata kidole baada ya mwathirika kukinga mkono ili asikatwe kichwa.

Mwanasheria huyo wa Serikali alidai kuwa kisa cha Ikonga kumkata Iddi ni kutokana na mshtakiwa na Ikonga kwenda katika katika grosari ya Iddi kunywa Pombe yenye thamani ya Sh. 23,000 na kuondoka bila kulipa.

Hatua hiyo, alidai kuwa, ilimfanya Iddi kumfuata na kuanza kumdai na hapo ndipo Chacha alipodai kuchukizwa kwa kumdai mbele za watu ndipo akaamua kuchukua uamuzi huo ambao umemsababishia mdai ulemavu wa kudumu.

Akitoa hukumu hiyo, Jaji Kahozya alisema: Kutokana na ushahidi uliotolewa katika mahakama hii kwa pande zote, naungana na upande wa mashitaka kwa kumtia hatiani Ikonga Chacha Ikonga kwa kosa la kumsababishia madhara Tatu Iddi kwa kumkata kidole cha mkono.

Kwa kosa hilo, utakwenda jela miaka 12 na kulipa fidia ya Sh. milioni mbili kwa Tatu ili iwe fundisho kwa watu wengine wanaojichukulia sheria mikononi kwa kudhuru watu wengine.

Pia ninatoa onyo kwa watu wanaochukua mali za wengine na wanapodaiwa wanawadhuru wale wenye haki ya kudai haki zao."



Mafundi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira mjini Shinyanga (SHUWASA), wakiendelea na utengenezaji wa mabomba juzi, ili kutoa huduma bora ya maji safi na salama kwa wananchi wa mjini humo. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Mchakato ujenzi barabara ya juu Jangwani waanza

**Na Beatrice Moses**

WAKALA wa Barabara (TANROAD), umeanza mchakato wa kutekeleza mradi wa kuinua Barabara ya Morogoro eneo la Jangwani ambalo limekuwa likifungwa barabara hiyo kila mara wakati wa mvua.

Meneja wa Wakala huo Mkoa wa Dar es Salaam, Ngusa Julius, alibainisha kuanza kwa mradi jana alipozungumza na Nipashe kuhusu suluhisho la adha inayoendelea kuwatesa watumiaji wa barabara hiyo hasa mvua inaponyesha kwa wingi na kusababisha Mto Msimbazi kukata mawasiliano ya barabara.

"Kuna mkandarasi amekuwa akifukua mchanga na tope pale ili kutoa nafasi maji yaweze kupita, bado hakuna mafanikio, kilichopo sasa ni kusubiri upembuzi wa mradi huo ukamilike kisha hatua nyingine zifuate kwa ajili ya utekelezaji," alisema.

Katika eneo hilo, maji ya mvua kutoka maeneo mbalimbali ya jiji hilo la kibiashara, yamekuwa yakifurika hivyo kuwaweka hatarini watumiaji wa barabara hiyo na mara nyingi Jeshi la Polisi limekuwa likiifunga barabara hiyo katika kipande cha Jangwani.

Hatua hiyo ya Jeshi la Polisi inasababisha usumbufu na gharama kubwa za usafiri.

Richard Abel, mkazi wa Kibamba jijini, alisema hulazimika kuunganisha magari matatu kwa safari moja ili kufika Posta anakofanya kazi.

"Serikali ione jinsi ambavyo inaweza kuhakikisha mpango huo unaanza na kuamilika mapema, hii kero ni kubwa, mbali na kutusababishia gharama, pia inasababisha tutumie muda mwingi kufika mjini na hata kurejea kwenye makazi yetu," alisema.

Juzi, Mkurugenzi wa Jiji la Dar es Salaam, Sipora Liana, alisikika akizungumzia suala hilo wakati akizungumza na moja ya vituo vya redio jijini, kwamba mpango huo ulitarajiwa kuanza mwaka huu ukihusisha Jiji, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na Benki ya Dunia (WB), lakini kuibuka kwa virusi vya corona kulisababisha kusimama kwa muda kwa utekelezaji wake.

Mkurugenzi huyo alibainisha kuwa mpango huo ukikamilika, mbali na kuondoa adha kwa watumiaji, pia utabadili taswira katika eneo la Jangwani kwa kuwa litakuwa la kuvutia kwa ajili ya mapumziko, michezo na makazi ya watu.

# Mambo ya msingi hotuba ya JPM

**Na Waandishi Wetu**

RAIS John Magufuli, amelizindua Bunge la 12 huku akiainisha mambo ya msingi anayotarajia kuyafanya katika kipindi chake cha pili cha miaka mitano ijayo ya uongozi wake.

Alianika vipaumbele hivyo katika hotuba yake ya uzinduzi wa Bunge hilo jana jijini hapa, uliohudhuriwa na viongozi mbalimbali wakiwamo marais wastaafu.

Rais Magufuli alisema katika miaka mitano ijayo, wataendelea kutekeleza yale yaliyopo katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Katika hotuba yake hiyo, Rais Magufuli pia alibainisha kuihamisha wizara inayohusika na uwekezaji kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu kwenda Ofisi ya Rais, akisisitiza kuwa amefanya hivyo ili yeye mwenyewe ashughulike na wanaokwamisha uwekezaji nchini.

### MASUALA YA MUUNGANO

Rais Magufuli ambaye alitumia saa 1:22 kuwasilisha hotuba yake hiyo bungeni, alisema serikali inayapa kipaumbele kikubwa masuala yanayohusu Muungano, akiahidi kulinda na kudumisha tunu za taifa, yaani amani, umoja, mshikamano, uhuru wa nchi na Muungano.

"Ninakuahidi Rais Dk. Hussein Mwinyi, miaka mitano ijayo Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itatoa ushirikiano wa karibu viziwani Zanzibar, tutafanya kazi kwa pamoja kwa lengo la kuleta maendeleo kwa pande zote mbili. Nitampa ushirikiano wa kutosha kutekeleza yote aliyoahidi wakati akifunguka Baraza la wawakilishi," alisema.

### UTAWALA BORA

Rais Magufuli pia alisema wataliimarisha eneo hilo hususani katika kusimamia nidhamu kwa watumishi wa umma na kuzidisha mapambano dhidi ya rushwa, wizi, ufisadi na ubadhirifu wa mali za umma.

"Kwenye miaka mitano ijayo, tutaendelea kushughulikia matatizo hayo. Na kwa kifupi, niseme utumbuaji majipu utaendelea. Tutaendelea kuboresha mazingira ya kazi pamoja na maslahi ya watumishi wetu wote ili yaendane na hali halisi ya maisha ya Watanzania. Kwa hiyo, watumishi wasiwe na wasiwasi," aliahidi.

### SEKTA YA UCHUMI

Alisema wamejipanga kuendeleza jitihada za kukuza uchumi na kwamba katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, walijitahidi kuisimamia na kukua kwa wastani wa asilimia saba kwa mwaka.

Rais Magufuli alisema wameongeza jitihada za kuwawezesha wananchi kiuchumi kwa kuwapatia mikopo isiyo na riba na yenye riba nafuu, ikiwamo mikopo ya asilimia 10 inayotolewa na halmashauri na kupitia Mifuko na programu mbalimbali zilizoanzishwa na serikali, ambayo kwa idadi zipo 18.

### SEKTA BINAFSI

Rais Magufuli alisema katika kipindi cha miaka mitano ijayo, sekta binafsi itapewa umuhimu wa pekee kwa kuhakikisha mtu yeyote atakayetaka kuwekeza, asisumbuliwe kwa kuwekewa vikwazo vya aina yoyote.



Rais Dk. John Magufuli, akiingia kwenye ukumbi wa Bunge. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

"Watanzania ni matajiri lakini baadhi yao wanasita kuwekeza hapa nchini kwa kuogopa kusumbuliwa na maswali yasiyo na msingi.

"Tunahitaji kuwa na mabilionea wengi wa Kitanzania. Ninataka Watanzania wote washiriki kikamilifu katika kujenga uchumi wa nchi yao," alisema.

### SEKTA YA KILIMO

Rais Magufuli alisema wanakusudia kuongeza tija na kukifanya kilimo kuwa cha kibiashara, lengo likiwa kujihakikishia usalama wa chakula, upatikanaji wa malighafi za viwandani na pia kupata ziada ya kuuza nje.

"Tutahakikisha pembejeo na zana bora za kilimo, ikiwamo mbegu, mbolea, viuatilifu, dawa na matrekta, vinapatikana kwa uhakika na kwa gharama nafuu. "Tutaongeza pia eneo la umwagiliaji kutoka hekta 561,383 hadi hekta milioni 1.2 mwaka 2025 ili kupunguza utegemezi kwenye mvua," alisema.

### MIFUGO, UVUVI

Alisema Tanzania inashika nafasi ya pili kwa mifugo barani Afrika kwa kuwa na ng'ombe milioni 33.4; mbuzi milioni 21.3; kondoo milioni 5.65; punda 657,389 ingawa sekta hiyo haijainufaisha nchi vya kutosha.

"Tunakusudia kuikuza sekta hii ili ichangie ukuaji uchumi na kupunguza matatizo ya umaskini na ukosefu wa ajira nchini. Tutaongeza maeneo ya ufugaji kutoka hekta 2,788,901 za sasa hadi hekta 6,000,000.

"Tutahamasisha ufugaji wa kisasa; tutaongeza vituo vya kuzalisha mbegu bora na pia kuongeza uzalishaji wa chakula cha mifugo viwandani kutoka tani 900,000 hadi milioni 8.

### SEKTA YA VIWANDA

Alisema miaka mitano iliyopita, walifanikiwa kujenga viwanda vipya takribani 8,477 ambavyo vilitengeneza ajira zipatazo 480,000 huku Mkoa wa Pwani ukiongoza kwa kujenga vingi.

"Tutaendeleza jitihada za kukuza sekta hii. Mkazo mkubwa tutauweka kwenye viwanda vyenye kutumia malighafi zinazopatikana kwa wingi hapa nchini (mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi); vyenye kuajiri watu wengi; na ambavyo bidhaa zake zinatumika kwa wingi Tanzania mfano nguo, bidhaa za ngozi, mafuta ya kula, sukari na saruji," alisema.

### SEKTA YA MADINI

Rais Magufuli alisema wanakusudia kuendelea kufanya majadiliano na wawekezaji wakubwa kwa kuzingatia mfano wa makubaliano yaliyofikiwa kati ya serikali na Kampuni ya Barrick yaliyowezesha kuundwa kwa Kampuni ya Twiga.

Alisema miaka mitano ijayo, wataendelea kuliimarisha Shirika la Taifa la Madini (STAMICO) ili lishiriki kikamilifu kwenye shughuli za madini; kuwawezesha wachimbaji wadogo, ikiwa ni pamoja na kuwatengea maeneo ya uchimbaji, kuwapatia mafunzo, mikopo pamoja na vifaa.

"Wapo baadhi ya watu wamepewa leseni za utafiti na uchimbaji lakini hawajazifanyia kazi; tutazifuta leseni zao, na maeneo hayo kuyagawa kwa wachimbaji wengine, hususan wachimbaji wadogo. Tutaimarisha masoko ya madini," alisema.

### SEKTA YA UTALII

Kuhusu sekta hii, Rais Magufuli alisema: "Tumejipanga kuongeza idadi ya watalii hadi kufikia milioni tano mwaka 2025 na mapato kutoka Dola za Marekani bilioni 2.6 za sasa hadi Dola za Marekani bilioni sita.

"Hatua tutakazochukua ni pamoja na kupanua wigo wa vivutio vya utalii, ikiwamo kukuza utalii wa mikutano na uwindaji wanyamapori; kuimarisha utalii wa fukwe; kujenga miundombinu ya kuwezesha meli za utalii kuzuru nchini na kuongeza kasi ya utangazaji wa vivutio."

### SEKTA YA NISHATI

Alisema ili kukuza uchumi, ni lazima waimarishe miundombinu, hususan ya usafiri na nishati ya umeme.

### SEKTA YA UCHUKUZI

Alisema watakamilisha ujenzi wa reli ya kisasa kutoka Dar es Salaam kwenda Dodoma na kuanza ujenzi wa vipande vya reli ya Mwanza - Isaka; Makutopora - Tabora; Tabora - Isaka - Tabora - Kigoma na Kaliua - Mapanda - Kalema, upanuzi wa bandari na ununuzi wa ndege nyingine tano.

### SEKTA YA MAWASILIANO

Alisema wamepanga pamoja na masuala mengine, kufikisha miundombinu ya Mkongo wa Taifa kwenye maeneo mengi ya nchi hususan wilayani.

"Tutawatambua na kuwasajili wataalam wote wa TEHAMA na tunakusudia kuweka anuani za makazi (postikodi) maeneo mbalimbali nchini. Tutaimarisha pia usalama kwenye masuala ya mawasiliano," alisema.

### AFYA, ELIMU

Rais Magufuli alisema kwa miaka mitano ijayo serikali yake inakusudia kuendeleza ujenzi wa miundombinu ya kutolea huduma za afya, hususan zahanati, vituo vya afya na hospitali za wilaya kwenye maeneo ambako hazipo.

Kuhusu sekta ya elimu, Rais Magufuli alisema serikali itaendelea kutoa elimu ya msingi na sekondari bila malipo, kuongeza bajeti ya mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu ili kuongeza idadi ya wanufaika.

### SEKTA YA MAJI

Rais Magufuli alisema kuna tatizo kubwa katika upatikanaji wa maji hasa maeneo ya vijijini, hivyo katika miaka mitano ijayo, nguvu itaelekezwa zaidi huko ili kuhakikisha fedha zinazopelekwa vijijini kutekeleza miradi ya maji zinatumika vizuri.

Alisema Mfuko wa Taifa wa Maji utaimarishwa ili kuuongezea uwezo wa kifedha wa kutekeleza miradi ya maji na miradi mikubwa itakamilishwa ukiwamo wa miji 28 utakaogharimu Sh. trilioni 1.2.

Alitoa wito kwa viongozi wote wakiwamo wabunge, kulifanya suala la kutunza vyanzo vya maji na miundombinu yake kuwa ajenda muhimu katika shughuli zao.

### DEMOKRASIA

Alisema wataendeleza jitihada za kukuza na kuimarisha demokrasia, kulinda uhuru na haki za wananchi na vyombo vya habari.

"Hata hivyo, ningependa kukumbusha kuwa lengo la demokrasia ni kuleta maendeleo na siyo fujo; na hakuna demokrasia isiyo na mipaka. Uhuru na haki vinakwenda sambamba na wajibu, hakuna uhuru au haki isiyo na wajibu, vyote vinakwenda sambamba," alisema.

### MAKUNDI MAALUM

Magufuli alisema miaka mitano ijayo wataendelea kuboresha mazingira ya kufanya biashara kwa wajasiriamali wadogo (machinga, mama lishe, baba lishe, waendesha bodaboda na bajaji).

"Kama mnavyofahamu, kwenye miaka mitano iliyopita, tulianzisha utaratibu wa kutoa vitambulisho maalum kwa wajasiriamali wetu wadogo. Miaka mitano ijayo, tunakusudia kuviboresha vitambulisho, ikiwamo kuweka picha na taarifa nyingine muhimu, kama ilivyo kwenye vitambulisho vya taifa au pasipoti.

"Hii itawawezesha wafanyabiashara watakaotumia vitambulisho hivyo kutambulika, ikiwamo kwenye benki na hivyo kupata mikopo kwa ajili ya kukuza biashara,"alisema.

Alisema watashughulikia masuala ya watu wa makundi maalum, ikiwamo wazee na watu wenye ulemavu na kuendeleza vita dhidi ya biashara haramu ya dawa za kulevya. Rais Magufuli alisema serikali itahakikisha wamiliki wa magari wanatoa mikataba kwa madereva ili kuipa hadhi inayostahili kazi hiyo na kuchochea shughuli za huduma za usafirishaji.

### SEKTA YA MISITU

Alisema wataimarisha sekta ya misitu na nyuki, ikiwamo kuanzisha viwanda vya mazao ya nyuki ili sekta hiyo itoe mchango mkubwa kwenye uchumi wa nchi na kuhamasisha ufugaji wa nyuki.

***Imeandaliwa na Augusta Njoji na Romana Mallya (DODOMA).**

HABARI KITAIFA

# TAMWA yataka mabadiliko Sheria Usalama Barabarani

**Na Beatrice Shayo**

CHAMA cha Wanahabari Wanawake Tanzania (TAMWA) na Mtandao wa Usalama Barabarani, wameiomba serikali kuhakikisha Sheria ya Usalama Barabarani inafanyiwa marekebisho kwa haraka ili kupunguza ajali nchini.

Akisoma tamko la pamoja la asasi hizo jana jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi wa TAMWA, Rose Reuben, alisema wanaamini maboresho ya sheria hiyo ambayo wamekuwa wakiipigia kelele kwa muda mrefu, yatasaidia kupunguza ajali za barabarani.

Wametoa tamko hilo ikiwa ni siku chache kabla ya kufanyika kwa maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Kuwakumbuka Waathirika wa Ajali za Barabarani inayofanyika Jumapili ya tatu ya Novemba kila mwaka.

Alisema mtandao huo unahimiza watunga sera kuendelea kubuni sera zitakazosaidia ushiriki wa mamlaka katika kudhibiti ajali barabarani.

"Tunashauri utafiti wa kina kufanyika baada ya ajali kutokea ili kujua namna ya kuzuia ajali hizo kutokea tena kwa siku zijazo," alisema Reuben.

Mkurugenzi huyo alisema kuna haja ya elimu kutolewa kwa wanafunzi shuleni kwa ajili ya kuwapa elimu ili wajue namna ya kusoma alama za barabarani.

"Tunasisitiza matumizi sahihi ya kofia ngumu, mikanda na viti vya watoto katika magari ili kulinda usalama na tunashauri madereva kuepuka mwendokasi barabarani," alisema.

Alikumbusha kuwa ripoti zinaonyesha ajali za barabarani zimepungua kwa kiasi kikubwa kutokana na kazi kubwa inayofanywa na asasi za kiserikali na zisizo za kiserikali katika kutoa elimu.

Reuben alisema mpaka sasa, mtandao wa wadau kutoka asasi za kiraia unaotetea marekebisho ya sheria na sera inayohusu usalama barabarani, unaendelea kutoa elimu kwa makundi mbalimbali.

Alisema kuwa kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa hivi karibuni na Ofisa Mrakibu Msaidizi wa Kikosi cha Usalama Barabarani, Deus Sokoni, mwaka 2017 ajali za gari zilikuwa 5,578, mwaka 2018 (3,732) na mwaka 2019 (2,704).

Alisema kwa taarifa hiyo, mwaka 2019 ajali zimepungua kutoka asilimia 35 hadi asilimia 28, vifo pia vimepungua kutoka asilimia 31 hadi asilimia 19 na majeruhi kutoka asilimia 32 hadi asilimia 20.

Reuben alisema gharama za majeruhi wa ajali duniani inasadikika kuwa ni Dola za Marekani bilioni 518 kila mwaka.

"Tunaamini kuwa ajali hizo zinaepukika kama dereva, wananchi na watumiaji wengine wa barabara watafuata sheria na kanuni za usalama barabarani," alisema Reuben.

Alibainisha kuwa katika kuadhimisha siku muhimu ya kuwakumbuka waathirika wa ajali za barabarani, wanaiomba serikali na watunga sheria kukubali na kupokea mawasilisho na mapendekezo yao ikiwa ni pamoja na kutunga sheria zinazopunguza kabisa ajali.

Mwathirika wa ajali ambaye ni Katibu Mkuu wa Chama cha Walioumia Uti wa Mgongo, Abdulaziz Shambe, alisema kuna haja serikali kuangalia uwezekano wa kuwasaidia waliopata ulemavu kutokana na ajali kupitia fedha za Mfuko wa Barabara.

" Huu mfuko unatengeneza barabara na sisi tunavyokwenda sheli tunakatwa fedha kwa ajili ya mfuko wa barabara. Je, wanatusaidia vipi waathirika?" Shambe alihoji.

Shambe alisema nchi nyingine huwa zinasaidia waathirika wa ajali, hivyo serikali iangalie uwezekano wa kusaidia hata kupatiwa matibabu bila malipo.

Ofisa Mradi kutoka Global Health Advocay Incubator, Hope Jasson, alisema wanaamini serikali ikiifanyia maboresho Sheria ya Usalama Barabarani ya Mwaka 1973 kwa kuzingatia maoni na mapendekezo ya wadau, ajali zitapungua zaidi.



Mwenyekiti wa Shirika la Wanawake katika Sheria na Maendeleo Afrika, (WiLDAF), Naomi Kaihula (wa pili kulia), akizungumza kwenye mkutano mkuu wa taasisi hiyo jijini Dar es Salaam jana. Wengine ni Mkurenzi wa WilDAF, Anna Kulaya (kulia), wajumbe wa bodi ya shirika hilo, Nakazael Tenga na Ebenezer Mshana. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

## Wauguzi wahamasishwa uelewa kuhusu kisukari

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI leo ni Siku ya Ugonjwa wa Kisukari Duniani, wauguzi wamehamasishwa kuwa na elimu sahihi ya ugonjwa huo.

Hayo yamo katika kaulimbiu ya mwaka huu juu ya ugonjwa huo inayosema: 'Wauguzi na Ugonjwa wa Kisukari'.

Taarifa iliyotolewa jana na Chama cha Ugonjwa wa Kisukari Tanzania (TDA) imesema wauguzi wakiwa na uelewa wa ugonjwa huo, itakuwa rahisi kuelimisha jamii juu ya kuudhibiti na kuutibu.

"Uelewa mzuri wa ugonjwa wa kisukari ndiyo ngome kuu ya kudhibiti na kuutibu ugonjwa huo," ilisema taarifa hiyo.

Miongoni mwa mambo ambayo taarifa hiyo inahimiza waaguzi wayaelewe ni pamoja na dalili za ugonjwa, madhumini na malengo ya matibabu.

Maana ya ugonjwa wa kisukari inaeleza kuwa ni mlolongo wa matatizo mwilini ya muda mfupi na mrefu kutokana na upungufu au kutokutumika vizuri kwa kichocheo kinachoitwa 'insulin'.

"Kichocheo hiki cha insulin kinahitajika ili mwili kutumia ipasavyo sukari," inaeleza sehemu ya taarifa hiyo.

Baadhi ya dalili za ugonjwa wa kisukari ni kiu ya mara kwa mara, kutoona vizuri, kukojoa mara kwa mara, kupungua uzito, uchovu wa mwili bila kufanya kazi na kuhisi kizunguzungu.

Shirikisho la Vyama vya Magonjwa Yasiyoambukiza (TANCDA) limeeleza kuwa katika kuadhimisha Siku ya Kisukari nchini, leo watafanya matembezi kutoka Hospitali ya Taifa ya Muhimbili hadi na Viwanja vya Mnazi Mmoja, Dar es Salaam.

Maadhimisho ya mwaka huu yamefanyika wakati inahitimishwa wiki ya Magonjwa Yasiyoambukiza (NCD).

Wiki ya NCD ilianza Jumatatu kwa kongamano la siku mbili la kisayansi ambalo ilitolewa taarifa na matokeo 200 ya utafiti uliofanyika nchini.

Matokeo ya utafiti huo yalijadiliwa na kuwekewa maazimio ya namna ya kuisaidia Tanzania katika kukabiliana na NCD.

# DC atengua uamuzi wakala wa maji

**NA FRANCIS GODWIN, IRINGA**

MKUU wa Wilaya ya Mufindi, Jamhuri Wiliam, ametengua uamuzi wa Wakala wa Maji Vijijini (RUSAWA) Wilaya ya Mufindi wa kuunda kamati za watumiaji maji katika miradi inayosimamiwa na taasisi isiyo ya kiserikali ya Rural Development Organization (RDO).

Licha ya kutengua uamuzi huo, ameagiza Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kuwachunguza viongozi wa RUWASA kwa tuhuma za ufisadi.

William alitangaza uamuzi huo juzi baada ya kupokea malalamiko kutoka kwa viongozi wa RDO kuhusiana na viongozi wa RUWASA kufika katika maeneo ya miradi ya maji na kuchochea migogoro kwa kuunda kamati zao tofauti na zile za RDO huku wakitaka wananchi kulipwa fidia kwa kutunza vyanzo vya maji.

Kutokana na malalamiko hayo, William katika mikutano yake iliyofanyika katika vijiji mbalimbali vya kata za Mdabulo Luhunga, mbali na kupiga marufuku RUWASA kuingilia na kuvuruga kazi inayofanywa na RDO, alitaka TAKUKURU kuchunguza zaidi ya Sh. milioni 20 zinazodaiwa kutumiwa na viongozi wa RUWASA kuzunguka vijijini kufanya vikao na wananchi kwa ajili ya kuunda jumuiya za watumiaji maji wakati tayari ziliundwa na RDO.

Alisema kilichofanywa na viongozi wa RUWASA ni kinyume cha utaratibu na kinakatisha tamaa wadau hao ambao wamejitolea kusaidia wananchi na kuwa kimsingi wananchi wanaozunguka miradi hiyo hawapaswi kulipwa fidia kwa kuwa miradi hiyo ni wananchi wenyewe na RDO wanasaidia serikali kusogeza huduma hiyo.

"RUWASA Mufindi leo (juzi) nataka niwape onyo kali. Katika kipindi kisichozidi mwaka mmoja, tumekwishawafuta kazi kazi mameneja wawili kutokana na utendaji kazi wao mbaya wenye kurudisha nyuma kasi ya serikali katika kuwahudumia wananchi kupata maji safi na salama," alisema.

William alisema ofisi yake imekuwa ikipokea taarifa juu ya RUWASA kupita kuunda vikundi vya jumuiya ya watumiaji maji kwa kutumia fedha za serikali wakati kwenye maeneo ambayo tayari RDO walikwishafanya kazi ya kuunda vikundi vya watumiaji maji kwa kutumia sera ya serikali ya maji .

Alisema kinara wa jambo hilo alikuwa ni fundi bomba ambaye hata elimu juu ya sera za maji hajui, hivyo ni lazima TAKUKURU kwenda kupiga kambi RUWASA ili kuchunguza fedha zilizotumika.

Sambamba na uchuguzi huo, alimtaka Meneja wa RUWASA kuacha mara moja vitendo vya uonevu dhidi ya wananchi na kuhakikisha kila mtumishi wa wakala anapangiwa kazi kulingana na elimu yake na si vinginevyo .

Awali, Mratibu wa RDO, Fidelis Filipatali, alimweleza mkuu huyo wa wilaya shabaha ya RDO katika kuendelea kusogeza huduma ya maji safi na salama kwa wananchi. Filipatali alisema pamoja na mafanikio makubwa waliyofikia katika kusogeza huduma ya maji, suala la siasa kuingizwa kwenye miradi ya maji limekuwa kikwazo kikubwa na kutaka miradi hiyo isiingizwe siasa ili kujiendesha.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Klabu Ligi Kuu Bara zitumie vyema kalenda ya kimataifa

**LIGI** Kuu Tanzania Bara imesimama kama zilivyo ligi nyingine duniani ili kupisha kalenda ya kimataifa ambayo hutumiwa na Timu za Taifa katika kusaka tiketi ya kufuzu kushiriki mashindano mbalimbali yatakayofanyika mwakani.

Ligi hiyo inayoshirikisha timu 18 lakini ndio hutoa mwakilishi wa Tanzania Bara katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika, inatarajiwa kuendelea tena ifikapo Novemba 20, mwaka huu.

Hii ni kwa sababu ya kutoa nafasi kwa kikosi cha Timu ya Taifa (Taifa Stars), kinachojiandaa na mechi dhidi ya wapinzani wao Tunisia (ugenini ilichezwa jana usiku na nyumbani itafanyika Novemba 17, mwaka huu), kumaliza majukumu yake.

Unaweza kusema ni likizo, lakini ni fursa nzuri kwa makocha kurekebisha upungufu uliyoubaini kwenye timu zao baada ya kucheza raundi 10.

Muda huu ni wa makocha na wachezaji ambao hawakufanya vyema katika mechi hizo zilizotangulia kwa sababu mbalimbali, kujipanga imara na hatimaye kurejea kwenye ligi wakiwa washindani na wenye makali.

Kama ambavyo baadhi yao wanasema bado ni mapema kutabiri bingwa wa msimu huu wa 2020/21, lakini 'Waswahili' wanasema biashara ni asubuhi, hivyo Nipashe inawakumbusha kutumia muda huu wa mapumziko kujipanga imara na hatimaye kujiepusha na janga na kushuka daraja.

Timu ambayo itatumia muda huu kuwajenga wachezaji wake vyema, itajiweka kwenye nafasi nzuri ya kurejesha makali na kuwa moja ya timu imara zenye nafasi ya kutwaa ubingwa au kukaa katika nafasi salama.

Ni mapema sana kukata tamaa na wakati huu ni muafaka kwa viongozi, makocha na wachezaji kuamini matokeo waliyonayo sasa hayawezi 'kupinduliwa', la hasha lolote linaweza kutokea katika mechi zilizosalia na mwisho wa msimu tukashuhudia bingwa asiyetarajiwa na kuona pia klabu zilizoonekana imara zikateremka daraja.

Soka ni sawa na marathoni, kuna wakati hatima ya bingwa wa msimu hupatikana siku ya funga pazia na timu zinazoshuka daraja pia zikajulikana katika siku hiyo ya mwisho.

Lakini ili kujiondoa kwenye 'presha' hiyo, huu ndio wakati wa kujipanga kuhakikisha kila timu inafikia malengo yake kwa kufanya vyema kwenye kila mchezo watakaocheza na kuacha tabia ya kudharau baadhi ya wapinzani wao.

Gazeti hili linawakumbusha jambo hili kwa sababu baadhi ya klabu zimekuwa zikionekana kujipanga kufanya vyema pale zinapocheza na vigogo ( Simba na Yanga), lakini hurejea kwenye utaratibu wake wa 'bora liende' pale zinapokutana na timu nyingine.


Hii si sawa, tunasema hivi kwa sababu tunaamini mechi zote za Ligi Kuu Tanzania Bara zina uzito unaofanana na klabu haiwezi kuwa bingwa kwa kupata matokeo chanya pale inapokutana na klabu hizo mbili za Kariakoo.

Viongozi, wachezaji na makocha ni vyema mkaachana na tabia hii endapo mnataka kufanya vizuri, kutoipa kipaumbele baadhi ya mechi ni kujishusha nyinyi wenyewe na inapokaribia mwisho wa msimu, klabu zinaanza kupata tabu kwa kusaka pointi za kuwanusuru na janga la kushuka daraja.

Vile vile kwa Simba na Yanga, umuhimu na maandalizi mnayoyaweka wakati mnajiandaa kukutana, yanatakiwa yawe na kiwango kinachofanana hata pale unapokutana na klabu nyingine, ili uwe bingwa ni lazima upate pointi nyingi, na pointi hizo hupatikana kutoka kwenye michezo yote.

Timu tano zilizokuwa juu kwenye msimamo hadi ligi hiyo inasimama ni pamoja na Azam FC yenye pointi 25, Yanga (pointi 24), mabingwa watetezi, Simba (pointi 20), Biashara United (pointi 17) na Ruvu Shooting inayonolewa na Mzalendo Boniface Mkwasa huku zile zinazoburuza mkia ni Gwambina FC, Mwadui FC, Kagera Sugar, Mbeya City na Ihefu FC.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Barnabas Maro

## Muungwana Lazima Nilonge

# Kandanda na maajabu yake

**"KILA** mvuvi wa pweza tutaonana mwambani." Pweza ni aina ya samaki mwenye umbo la duara lililozungukwa na mikono au minyiri minane.

Kwa kawaida wanaovua samaki hukutana mwambani au mahali pa kuvulia.

Methali hii hutumiwa kupigia mfano watu wanaofanya kazi au majukumu yanayoingiliana na ambao kwa namna yoyote ile lazima wakutane. Huweza pia kumtambia mwingine anayejidai kuwa na ujuzi fulani, kumkumbusha kwamba ujuzi wake utaonekana wakati ukifika.

Vile vile "Kila ngoma ina mchezo wake" kwani huwa na namna yake ya kuchezwa. Hii ina maana kuwa kila jambo huwa na mbinu na taratibu zake za kulifanyia. Mchezo wa mpira wa miguu wenye majina mengi, yaani kandanda, kabumbu na soka wakati mwingine huwa na matokeo ya kushangaza.

Timu yoyote hucheza ili ishinde; sio kushindwa. Tumeona kwa njia ya runinga au kusoma magazetini jinsi timu maarufu duniani zikifungwa na timu zisizotarajiwa ingawa zote zipo kwenye ligi moja.

Wahenga walisema "Ngoma ikivuma sana hupasuka." Maana yake ngoma ivumayo sana kutokana na kupigwa huishia kupasuka. Methali hii hutumiwa kutukumbusha kwamba jambo lolote huharibika, hasa linapopita kipimo chake.

Tuchukue mfano wa timu za wenzetu kule Ulaya kama Manchester United, Arsenal, Chelsea, Liverpool, Barcelona, Real Madrid n.k. zilivyotamba zamani lakini sasa zaonekana kuwa timu za 'kawaida' tu hivyo kufungwa si ajabu. Sembuse timu za Tanzania?

Hapa nchini, timu zilizotikisa kwa muda mrefu ni Yanga na Simba lakini sasa zashindwa hata na timu zinazoitwa 'ndogo' zinazozichachafya (nyanyasa, zidi nguvu; hangaisha).

Wahenga walituachia methali isemayo "Hakuna kubwa lisiloshindwa." Maana yake hakuna jambo lisilowezekana. Hutumiwa kumhimiza mtu anayekabiliana na hali ngumu kuwa lazima atafanikiwa hatimaye. Ligi Kuu ya msimu huu yenye timu 18 imekuwa na maajabu yasiyotarajiwa. Kwa upande mmoja timu zinazoitwa 'ndogo' zinaelekea kuzichachafya timu ziitwazo 'kubwa' yaani Azam, Simba na Yanga.

Timu hizo 'ndogo' zimetoa sare na kuzifunga 'kubwa' kwa mshangao wa wengi! Kumbe penye nia pana njia. Kwamba mtu akiwa na dhamira ya kulifanya jambo hawezi kuikosa njia. Timu ngeni msimu huu ni Dodoma Jiji, Gwambina FC, na Ihefu zilizopanda daraja.

Mpaka sasa timu zote zimecheza michezo 10 kila moja zikiongozwa na Azam iliyoshinda michezo 8, kupata sare moja na kufungwa mechi moja. Ina mabao 18 ya kufunga, manne ya kufungwa na alama 25.

Yanga inafuatia kwa idadi hiyo hiyo ya michezo ikishinda michezo 7, sare tatu bila kupoteza mchezo wowote. Ina mabao 12 ya kufunga , matatu ya kufungwa na kupata alama 24. Moja nyuma ya Azam.

Simba ambayo inatetea nafasi yake ya ubingwa kwa mara ya nne, inafuatia katika nafasi ya tatu ikishinda mechi 6, sare mbili, kufungwa michezo miwili ikiwa na idadi ya mabao 22 ya kufunga. Imefungwa mabao matano na kupata alama 20.

Kipigo cha Simba kufungwa mara mbili mfululizo dhidi ya Tanzania Prisons na Ruvu Shooting kimewashangaza wengi hata kufanya baadhi ya viongozi wao kusema maneno yasiyoridhisha kwa baadhi ya wachezaji wao.

Mshangao mwingine ni timu machachari za Coastal Union ya Tanga ikiwa nafasi ya 10, Mtibwa Sugar ya Morogoro ikiwa nafasi ya 12, Kagera Sugar ya Kagera katika nafasi ya16 na Mbeya City kwenye nafasi ya 17 zinaacha maswali: "Zimekumbwa na kitu gani? Kwa nini zimeporomoka kiasi hicho?" Mchezo ni jambo ambalo watu au timu hufanya kwa kushindana ili kupata mshindi; jambo linalofanywa kwa nia ya kuburudisha.

Ukweli huo ndio unaowafanya wachezaji wacheze kwa ari, yaani moyo wa kutaka kufanya jambo bila kushindwa; shauku, hamu, shime. Wanaocheza chini ya kiwango, yawezekana huamka na mavune, yaani hali ya uchovu wa mazoezi magumu. Kuwalaumu ni kuwaonea kwani wao ni binadamu na wanachoka kama sisi tunapofanya kazi ngumu.

Tusiwalaumu wala kuwakatisha tamaa wachezaji kwani wanapokuwa uwanjani ni eneo lao la kazi wakati wewe ukishangilia na kulaumu bila kujua magumu wanayokumbana nayo.

Kazi ni shughuli kama vile kilimo, ukarani, ualimu na kadhalika ambayo mtu hufanya ili kujipatia riziki ya kuendesha maisha yake. Ndivyo ilivyo kwa wacheza kabumbu na ndivyo walivyo kama wewe unavyojali kazi inayokupa mkate wako wa kila siku.

**marobarnabas@yahoo.com**
**0784 334 093**

HABARI PICHANI

# UZINDUZI WA BUNGE LA 12 JIJINI DODOMA



Rais Dk. John Magufuli, akikagua gwaride maalum lililoandaliwa kwa ajili yake, kabla ya kuli-hutubia na kulizindua Bunge la 12, jijini Dodoma jana. **PICHA ZOTE: IBRAHIM JOSEPH**



Rais Dk. John Magufuli, akiingia kwenye ukumbi wa Bunge.



Kutoka kushoto; Jaji Mkuu wa Tanzania Prof. Ibrahim Juma, Jaji Mkuu wa Zanzibar, Omary Makungu, Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Zuberi Ali Maulid na Spika wa Bunge la Afrika Mashariki, Martin Ngoga, wakifuatilia hotuba ya Rais Dk. Magufuli.



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi (wa pili kulia), Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar, Hemed Suleiman na Naibu Spika, Dk. Tulia Ackson walifua-tilia uzinduzi wa Bunge hilo.



Viongozi wa vyama vya siasa wakifuatilia hotuba ya Rais Dk. Magufuli ndani ya ukumbi wa Bunge.



Baadhi ya wageni mbalimbali wakiwa ndani ya ukumbi wa Bunge.

## Kikongwe apewa ardhi aliyoporwa

**Na Richard Makore,**
MWANZA

HATIMAYE baada ya takribani miaka 10, Baraza la Ardhi na Nyumba Wilaya ya Mwanza, limetoa hukumu na kumpa haki ya umiliki wa eneo alilokuwa ameporwa bibi kikongwe Anastazia Ndazi mwenye umri zaidi ya miaka 90.

Anastazia, mkazi wa mtaa wa Bwiru Ziwani uliopo katika Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela mkoani Mwanza, alipata haki hiyo jana katika uamuzi uliotolewa na Mwenyekiti wa Baraza hilo, Mayeye Sigiti, na kumwamuru Yohana Magayane kuhama na kuachia eneo hilo.

Aidha, baraza hilo limemwamuru Magayane kumjengea Bibi hiyo nyumba aliyobomoa na kuondoka eneo hilo.

Akizungumza nje ya baraza hilo, Wakili wa Bibi huyo, Gasper Mwanalyela, alisema kesi hiyo ilichukua muda mrefu hatimaye haki imepatikana .

Wakili Mwanalyela alilishukuru baraza hilo kutenda haki kwa bibi Anastazia huku Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Kivulini, Yassin Ally, akisema utekelezaji wa hukumu hiyo utakwenda kwa kasi.

Alisema shirika lake lilimwekea Wakili bibi huyo ili apate haki yake na kwamba shirika limekuwa mstari wa mbele kutetea watu wanaoporwa haki zao kwa kutumia uwezo wa mabavu au fedha

Hata hivyo, Magayani aliyetakiwa kurudisha ardhi ya kikongwe huyo pamoja na kumjengea nyumba yake aliyoibomoa, ameonyesha kutoridhishwa na hukumu hiyo na kuahidi kukata rufani.

# Kilo 242 dawa za kulevya zateketezwa

**Na Hellen Mwango**

JUMLA ya kilo 242.106 za dawa za kulevya zikiwamo heroin, cocaine na bangi, zimeteketezwa baada ya mahakama kusikiliza na kutoa hukumu katika kesi mbalimbali na kuamuru dawa hizo kuteketezwa.

Tume ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya nchini, iliteketeza heroine kilo 118.174, cocaine kilo 3.932 na kilo 120 za bangi, jijini Dar es Salaam.

Tukio hilo lilifanyika katika viunga vya Kiwanda cha Saruji cha Twiga, Wazo jijini Dar es Salaam chini ya Mkurugenzi wa Mashitaka (DPP), Biswalo Mganga; Kamishna wa Ukaguzi na Sayansi Jinai wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Bertha Mamuya, mawakili wa kujitegemea na maofisa kutoka Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC).

Akizungumza kabla ya tukio hilo kuanza, Jaji wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Edwin Kakolaki, alisema vielelezo vyote vinavyopokewa mahakamani na kutumika kama sehemu ya ushahidi na kupokewa kama kielelezo pindi kesi zikiwa zimeisha, huteketezwa kwa amri ya mahakama.

"Wapo watu wanajiuliza vielelezo vinavyopokewa mahakamani baada ya kesi kutolewa hukumu vinakwenda wapi. Huwa vinateketezwa na zile tetesi za kwamba mashauri yake yakiisha huwa vinarudi mitaani si za kweli.

"Dawa hizi zinateketezwa kutokana na amri ya mahakama baada ya kesi kufika mahakamani, kusikilizwa na kumalizika kisha kupokewa kama kielelezo cha mahakama na baadaye hutoa amri ya kuteketezwa," alisema Jaji Kakolaki.

Alisema katika tukio zima la kuteketeza wa dawa za kulevya, lazima wawepo mashuhuda ili kushuhudia amri ya mahakama jambo ambalo kufanyika kwa uwazi ili Watanzania wajue kesi inapoenda mahakamani na kumalizika lazima vielelezo viteketezwe kwa uwazi.

DPP Mganga alisema dawa zilizoteketezwa juzi zilitokana na kesi 15 zilizofikishwa mahakamani na kumalizika.

Aidha, alisema Oktoba, mwaka jana, kilo 10.65 za cocaine na kilo 226.149 za heroin zilizotokana na kesi 17 ziliteketezwa na tangu mwaka jana, jumla ya kilo 345.22 za heroin zimeteketezwa, kilo 14.5 za Cocaine na bangi kilo 120 zikihusisha kesi 32 kwa Mkoa wa Dar es Salaam pekee.

Alisema kesi iliyokuwa na dawa za kulevya nyingi ni uhujumu uchumi namba 14/2018 iliyowahusisha raia 12 wa Iran waliokutwa na kilo 111.02 za dawa za kulevya aina ya heroine ambayo imemalizika hivi karibuni na wawili wamehukumiwa na Mahakama Kuu ya Tanzania, Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi kutumikia kifungo cha miaka 30 jela.




Askari wa Kikosi cha Usalama Barabarani, akimuandikia adhabu dereva wa gari dogo baada ya kuendesha katika barabara ya mabasi ya mwendo kasi, eneo la Jangwani, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# TAWA yawanoa watumishi kuhusu rushwa

**Na Christina Haule,**
MOROGORO

MAMLAKA ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA) imetoa elimu kuhusu rushwa kwa watumishi 351 kutoka kwenye vituo vyake 15 katika kipindi cha Julai hadi Oktoba, mwaka huu.

Lengo la mafunzo hayo ni kuwawezesha wafanyakazi hao kukabiliana na matukio ya rushwa na ujangili ambayo yamekuwa wakifanywa.

Kaimu Kamishna wa Uhifadhi TAWA, Mabula Nyanda, alisema hayo juzi wakati akimkaribisha Katibu Mkuu Wizara ya Maliasili na Utalii, Dk. Aloyce Nzuki, kufungua kikao cha menejimenti ya mamlaka makao makuu na wakuu wa vituo vya hifadhi, kilichofanyika mjini hapa.

Alisema mamlaka imekuwa ikichukua hatua mbalimbali katika kukabiliana na matukio hayo kwa kushirikiana na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU).

Nyanda alisema katika kupambana na hali hiyo, TAWA imeweka utaratibu wa kutembelea vituo kuhimiza utendaji kazi, kutoa elimu kuhusu maadili ya utumishi wa umma na kujiepusha na rushwa.

Alisema katika kuchukua hatua kwa mujibu wa Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai katika kipindi cha Desemba hadi Agosti, mwaka huu, watumishi 53 walifikishwa vituo vya polisi kwa tuhuma za rushwa.

Nyanda aliitaja idadi ya watumishi, mapori wanayotoka na idadi yao kwenye mabano kuwa ni Maswa (11), Swagaswaga (tisa), Moyowosi (wanane), Rungwa/Muhesi/Kizigo (130, Liparamba (wawili), Selous (watatu), Kanda za Kikosi Dhidi ya Ujangili (KDU) Bunda (sita) na Manyoni mmoja.

Nyanda alisema mamlaka inaamini kuwa hatua hiyo inaathiri utendaji kazi kwa kuwa inapunguza idadi ya watumishi na kwamba wakati wote imekuwa ikichukua taahadhari ya uchunguzi wa kina kabla ya kuchukua hatua.

Pia alisema katika kutekeleza hatua za kinidhamu kwa mujibu wa sheria na kanuni za utumishi wa umma, mamlaka imeunda kamati za nidhamu tano katika mwaka wa fedha 2019/20 lengo likiwa ni kuchunguza masuala ya kinidhamu kwa watumishi.

Akifunga kikao hicho, Dk. Nzuki alisema wizara kwa kushirikiana na TAWA iko katika hatua mbalimbali za kutatua baadhi ya matatizo yanayoiakabili mamlaka hiyo, ikiwamo uhaba wa watumishi kwenye baadhi ya fani zikiwamo sheria, uhasibu na uhandisi.



# Kampuni ya Uturuki yaonyesha nia kuwekeza sekta ya madini

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KATIBU Mkuu Wizara ya Madini, Prof. Simon Msanjila, jana alikutana na kufanya mazungumzo na kampuni ya AGA Bullion kutoka Uturuki iliyoonyesha nia ya kutaka kuwekeza kwenye sekta ya madini nchini.

Katika kikao hicho kilichofanyika ofisini kwake, Mtumba jijini hapa, Prof. Msanjila aliieleza kampuni hiyo uwapo wa masoko ya madini yaliyoanzishwa kila mkoa hususani ile yenye uzalishaji mkubwa wa rasilimali hiyo.

Mikoa hiyo ni pamoja na Geita, Mwanza, Kahama, Chunya, Arusha na kwingineko ambako AGA Bullion watawekeza kwa kununua na kuuza madini kwenye masoko ya nje.

Prof. Msanjila, aliitaka AGA Bullion kuwafikia wachimbaji wadogo na wa kati kwa kuwapa uzoefu wa uwekezaji katika sekta ya madini.

Pia alitaka kampuni hiyo kutembelea mgodi wa dhahabu wa Geita na Busolwa, ambao ni mgodi wa kati unaofanya uwekezaji katika uchimbaji wa madini ya dhahabu vizuri hapa nchini.

Alisisitiza kuwa uwekezaji unaopangwa kufanywa na AGA Bullion usilenge kwenye biashara ya madini ya dhahabu pekee bali kwenye madini mengine yanayopatikana nchini ikiwamo Tanzanite yanayopatikana mkoani Manyara.

Vilevile, Prof. Msanjila aliitaka kampuni hiyo kuomba leseni ya uchimbaji madini ili kuanza kazi hiyo nchini.

Kadhalika, aliitaka AGA Bullion kukutana na wadau mbalimbali wa sekta ya madini lilikwamo Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) ambao hutoa huduma na ushauri wa kitaalam kwa wachimbaji wadogo, uchenjuaji dhahabu, kununua na kuuza madini.

Mkurugenzi Mwanzilishi wa AGA Bullion, Sarp Tarhanaci alimweleza Prof. Msanjila kuwa kampuni hiyo inamiliki viwanda viwili vya usafishaji wa dhahabu katika nchi za Umoja wa Falme za Kiarabu (Dubai) na Uturuki.

Pia alielezea uzoefu wao katika ununuzi wa dhahabu kutoka mataifa mbalimbali kama vile Ghana, Burkina Faso, Peru, Malaysia na Uturuki.

Kuhusu kukutana na wadau wengine wa sekta ya madini, Tarhanaci alisema kampuni hiyo Novemba 10, mwaka huu, ilikutana na kufanya mazungumzo na Chama cha Wafanyabiashara wa Madini (TCME) na kupokea taarifa za uzalishaji na mauzo ya dhahabu.

Kadhalika Novemba 11, ilikutana na Mkurugenzi wa Masoko ya Kifedha wa Benki Kuu ya Tanzania ili kueleza nia yake ya kutaka kutoa huduma ya usafishaji wa dhahabu, bima na kutafuta masoko ya kimataifa ya dhahabu iliyosafishwa kwa gharama ya asilimia 0.5 hadi asilimia 0.8 ya thamani ya madini hayo.

Alisema AGA Bullion inayo dhamira ya kufanya biashara ya madini ya dhahabu kutoka wa wachimbaji wadogo, wachimbaji wa kati ikiwamo kuwawezesha kwa kuwapa mitaji ya fedha ili kuzalisha zaidi na kutoa mafunzo kwa wachimbaji.

"Pia tutakutana na Shirikisho la Vyama vya Wachimbaji Wadogo wa Madini (FEMATA) ili waweze kujadili mambo mbalimbali kwa pamoja" alisema

Aidha amezungumzia nia ya kampuni hiyo kusaidia viwanda vya uongezaji thamani madini ya dhahabu (masonara) kwa kutengeneza bidhaa zake kama vile pete, hereni na mikufu.

Kikao hicho pia kulihudhuliwa na viongozi wengine waandamizi wa Wizara akiwemo Kamishina wa Madini, Mhandisi David Mulabwa, Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu, Issa Nchasi.



Ofisa Masoko wa Jiji la Dodoma, James Yuna (kulia), akizungumza na wafanyabiashara wa mbogamboga na matunda akiwataka kuondoka baada ya kuvamia eneo la stendi ya daladala ya Sabasaba na kusababisha magari kushindwa kuingia kwenye eneo hilo, jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# RC awaonyesha fursa viongozi wa dini

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge, amewataka viongozi wa madhehebu ya dini mkoani hapa, kuchangamkia fursa ya viwanja ambavyo vinatolewa na Halmashauri ya Jiji la Dodoma ili kuwekeza kwenye huduma mbalimbali.

Dk. Mahenge alisema hayo juzi alipokuwa akifungua mkutano wa maombi wa siku nne unaofanyika kwenye viwanja vya wajenzi jijini Dodoma, chini ya mhubiri wa kimataifa kutoka Marekani, Dk. Dana Morey.

Akizungumza na wananchi waliohudhuria kwenye mkutano huo, alisema katika jiji la Dodoma, kuna fursa ya viwanja vinavyotolewa kwa watu wote, wakiwamo viongozi wa dini.

Dk. Mahenge aliwashukuru viongozi wa madhehebu ya dini kwa kuhamasisha waumini wao kushiriki kikamilifu katika mchakato mzima wa uchaguzi mkuu 2020 na kupitia kwa amani na utulivu.

Alisema viongozi wa dini wamewezesha kwa kuwatumia waumini kuomba kwa muda wote ili uchaguzi huo uwe wa amani na utulivu, ikiwa ni pamoja na kuwahamasisha waliokuwa wamejiandikisha kujitokeza kwa wingi ili kutumiza haki ya kikatiba.

"Serikali inawapongeza kwa hili ambalo limepita kwa usalama kama vile ilivyokuwa kwenye kipindi cha maambukizi ya ugonjwa wa corona. Watanzania walijitokeza kwa pamoja kuomba na Mungu akatusikia na hatimaye ugonjwa huo umetoweka," alisema.

Dk. Morey kwa upande wake, aliwataka Watanzania kudumisha amani waliyo nayo ndani ya nchi kwa kumshirikisha Mungu zaidi.

Alisema Watanzania Mungu amewaletea amani hii ambayo nchi zingine zinatamani, hivyo anawaomba waitunze ili iwe mfano hata kwa mataifa mengine.

# Waliojenga vibanda watakiwa kuondoka

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

HALMASHAURI ya Jiji la Dodoma imewaagiza wafanyabiashara wote waliojenga vibanda kwenye maeneo yasiyo rasmi pembezoni na barabara katika stendi ya daladala ya Sabasaba kuondoka mara moja.

Aidha, maeneo mengine ambayo yanatakiwa kuwa wazi ni pamoja na pembezoni mwa majengo ya ofisi za serikali ambako kumejengwa vibanda ambavyo vinasababisha usumbufu kwa watumiaji wa maeneo hayo.

Ofisa Masoko wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma, James Yuna, alisema hayo jana alipokuwa akizungumza na wafanyabiashara wa mboga na matunda wa stendi ya Sabasaba pamoja na wale waliovamia na kuweka biashara zao kwenye maeneo ya barabara.


Akizungumza kwenye ziara yake hiyo ambayo aliitumia pia kutoa elimu na maelekezo kwa wafanyabiashara, alitaka maeneo yote yaliyovamiwa kuwa wazi kwa kuwa hayako rasmi na si salama kwa kufanya biashara.

Ofisa huyo alisema kuna makundi ya wafanyabiashara, wakiwamo wauza mboga, matunda na machinga wamevamia maeneo yasiyo rasmi na kukiuka kanuni, sheria na utaratibu uliowekwa na Halmashauri ya jiji. Alisema wafanyabiashara hao wameamua kuweka bidhaa zao bila kujali usalama huku wakitambua kuwa kufanya hivyo ni makosa.

"Mfano mzuri kama hapa stendi ya daladala Sabasaba, magari yanashindwa kupaki kwenye eneo lao kutokana na ninyi wafanyabishara wa mboga na matunda, hali ambayo inahatarisha maisha yenu, bidhaa na hata kwa wateja wenu mnaowahudumia, hivyo ninawaomba mpishe ili magari yapaki hapa," alisema.

Pia ofisa huyo aliwataka wafanyabiashara hao pamoja na kuwa na vitambulisho vyao visitumike vibaya kwa kuvunja sheria bila kujali maelekezo yanayotolewa na Halmashauri ya Jiji.

Alisema vitambulisho hivyo pamoja na kuwafanya wawe huru, wanatakiwa pia kutii sheria na maelekezo ambayo yanayowataka kufuata kanuni na sheria.



# Waanika matatizo ya wenye ulemavu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WALIMU wanaowafundisha wanafunzi wenye ulemavu wa uziwi, wamesema wanafunzi hao wanakabiliwa na matatizo mengi ikiwamo udhalilishaji wa kijinsia.

Akizungumza juzi katika mafunzo maalum ya lugha ya alama kwa wanafunzi wenye ulemavu huo na walimu wao yaliyofanyika Shule ya Mwanakwerekwe 'A' Unguja, mmoja wa walimu hao, Sabra Pande Khamis, alisema udhalilishaji wanaofanyiwa watoto hao, wazazi wao hushindwa kuwabaini kwa sababu wengi hawajui lugha za alama.

Sabra alisema kuwa baadhi ya wanafunzi wenye ulemavu wa uziwi wanapofanyiwa vitendo vya udhalilishaji katika jamii, hutoa taarifa kwa walimu wanaojua lugha ya alama ili kufahamiana.

Alisema kutokana na wazazi na walezi wengi kutojua lugha ya alama, wanafunzi hao hushindwa kuwaelezea matatizo yanayowakabili ikiwamo udhalilishaji.

"Wanafunzi wetu wenye ulemavu wa uziwi wanapokumbana na matatizo huja kutueleza sisi shuleni ili tuwasaidie," alisema.

Kutokana na tatizo hilo, aliwataka wazazi na walezi hao kujifunza lugha ya alama ili kuwa na mawasiliano mazuri na watoto wao na wanapopatwa na matatizo, kuwasikiliza na kuyafikisha katika sehemu husika ili kupatiwa ufumbuzi.

Pia alitoa wito kwa wazazi kuwa karibu na watoto wao hasa wenye matatizo hayo na kuwapa msaada unaohitajika kutokana na wanafunzi hao kuwa na uwezo wa kusoma na vipaji vya kujiendeleza ili nao wafikie malengo yao kama wanafunzi wengine.

Akitoa mada ya udhalilishaji, Mkuu wa Seksheni na Stadi za Maisha kutoka Kitengo cha Elimu Mjumuisho, Fatma Mbaraka Hashim, aliwataka Wanafunzi wenye mahitaji maalum kuzijua mbinu mbalimbali wanazotumia wadhalilishaji ili kujiepusha nazo wakati wahusika wanapotaka kuwafanyia vitendo hivyo.

Alisema wadhalilishaji wamekuwa wakitumia mbinu mbalimbali wanapotaka kuwadhalilisha watoto hasa kuwabaka ili lengo lao liweze kufanikiwa kwa urahisi.

Fatma alizitaja baadhi ya mbinu hizo kuwa, kuanza kuwaonesha picha za ngono, kuwashika katika sehemu za mwili wao, kuwakonyeza na hata baadhi yao kuwaonesha sehemu zao za siri, hivyo aliwataka kukaa mbali na watu hao.

# Wajumbe BLW wanolewa kuhusu wajibu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKUU wa Kitivo cha Sheria cha Chuo Kikuu cha Zanzibar, Dk. Yahya Khamis Hamad, amesema Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wana wajibu wa kutambua na kufuatilia kero na matatizo ya wananchi.

Kwa kufanya hivyo, watakuwa na uwezo wa kuyapatia ufumbuzi na kuleta maendeleo katika majimbo wanayoyawakilisha.

Akizungumza jana katika semina elekezi kwa wajumbe wa Baraza la Wawakilishi huko Chukwani, nje ya mji wa Zanzibar, Dk Yahya alisema miongoni mwa kazi za mwakilishi ni kufuatilia miradi ya maendeleo iliyokubaliwa kutekelezwa katika maeneo yao.

Dk. Yahya alisema katika kutimiza wajibu huo, wajumbe wa Baraza la Wawakilishi hawana budi kutenga muda na kufanya vikao na wananchi wa maeneo yao ili kuwapa fursa ya kubadilishana mawazo.

Alisema kwa kutumia nafasi hiyo, mjumbe anaweza kupata taarifa zitakazomwezesha kujua vipaumbele vya wananchi wa eneo lake na kufikisha taarifa hizo kwenye ngazi zinazohusika na utawala wa nchi kwa ajili ya kupatiwa ufumbuzi.

Kwa mujibu wa Dk. Yahya, kwa misingi hiyo, wajumbe wa Baraza la Wawakilishi lazima wapambanue kwa usahihi mambo yanayodaiwa na wananchi wa maeneo yao.

Kuhusu maadili ya mwakilishi, Dk Yahya alisema mjumbe anatakiwa wakati wote kuzingatia maadili ya kazi zake ili kulinda heshima ya baraza na taifa kwa jumla. Katika suala hilo, alisema mwakilishi ahakikishe hajiiingizi wala kujihusisha katika vitendo vinavyoweza kulidhalilisha Baraza.

Alivitaja baadhi ya vitendo hivyo ni pamoja na rushwa, kashfa au matumizi ya lugha ya matusi, mavazi yasiyoheshimu mila, desturi na utamaduni wa Wazanzibari na mambo yanayofanana na hayo.

Akitoa mada inayohusiana na historia na maendeleo ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Mkurugenzi wa Mashtaka, Ibrahim Mzee Ibrahim, alisema maendeleo makubwa yamepatikana ikiwa ni pamoja na kuongezeka kwa ushiriki wa wanawake.



Mkufunzi Safia Hashim Makame (kushoto), akiwafundisha wajasiriamali jinsi ya kutengeneza sabuni na viksi katika darasa maalum lililofanyika katika ofisi za chama cha waandishi wa habari wanawake Tanzania (TAMWA), upande wa Zanzibar juzi. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# ACT Wazalendo yataka tume kuchunguza uvunjifu wa haki

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

CHAMA cha ACT Wazalendo kimeshauri iundwe tume kuchunguza matukio ya uvunjifu wa haki za binadamu yaliyotokea Zanzibar. Akizungumza jana na waandishi wa habari, Mkurugenzi wa Haki za Binadamu wa chama hicho, Juma Abdallah, alisema kabla na baada ya uchaguzi mkuu wa Oktoba, mwaka huu, kuna matukio mengi ya uvunjifu wa haki za binadamu yalijitokeza.

Juma alisema matukio hayo waathirika wake zaidi ni viongozi na wanachama wa chama cha ACT Wazalendo ambapo baadhi yao wametekwa, wamepigwa na kufariki dunia.

Aidha alilitaka Jeshi la polisi kuchukua hatua za kisheria kwa wale wote wanauhusika kuwateka raia na baadae kuwatupa katika maeneo tofauti ambayo ni kinyume cha misingi ya haki za binadamu na utawala bora.

"Sisi ACT Wazalendo hatuwezi kunyamazia uporaji wa demokrasia, mauaji yaliofanywa, mateso yaliyowapata watu, kukamatwa watu na kutofikishwa mahakamani maana nafsi zetu zitatusuta na hatutotimiza wajibu wetu wa kikatiba," alisema.

Pia aliitaka serikali imfikishe haraka mahakamani Naibu Katibu Mkuu wa chama hicho, Nassor Ahmed Mazrui, au wamuachie yeye na wezake wanaoshikiliwa na Jeshi la Polisi.

Alisema wanapinga uamuzi wowote wa kuwapeleka Wanazibari Tanzania Bara kwa kosa lolote kwa sababu Mahakama ya Zanzibar ina mamlaka kamili.

Juma alisema uchaguzi mkuu ulikuwa wa nguvu na vitisho na kwa mujibu wa maelezo yake, watu 15 Unguja na Pemba wapigwa na kufariki dunia na watu 150 wamepigwa na kudhalilishwa.

Naye Mwanasheria kutoka chama hicho, Omar Said Shaaban, alisema wamepeleka ombi Mahakama Kuu ya Zanzibar kuomba kutoa amri kwa Jeshi la Polisi kuwaachia Mazrui na Ayoub Bakari au wawapeleke mahakamani kuwashtaki kwa mambo wanayotuhumiwa kuwa nayo.

Alisema ombo hilo limesikilizwa juzi upande mmoja na mahakama imekubaliana na wao kuwa upande wa pili wanaowashtaki ambao ni Kamishna wa Polisi Zanzibar na Naibu Mkurugenzi wa makosa ya Jinai ambao walitakiwa kuwapo mahakamani juzi lakini hakufika na waliwatuma wanasheria wao.

Omar alisema katika maelezo ya ombi lao Mahakama Kuu Zanzibar, walieleza kuwa wanayo sababu ya kujibu viapo vilivyoambatanishwa na ombi lao na kutaka wapewe muda wajibu kwa maandishi.

Alisema baada ya majadiliano ya pande zote mbili, Mahakama imetoa amri kwamba wahusika wafanye majibu ya viapo vyao Novemba 16, mwaka huu, na ombi lao litasikilizwa Novemba 17 ambapo Mahakama itatoa uamuzi wa maombi ya amri wanazoziomba kuwaachia viongozi wa ACT au kuwashtaki mahakamani.





JUMAMOSI NOVEMBA 14, 2020



VITA KAMILI

# Harmonize vs Diamond

WIMBO mpya wa mwanamuziki nyota nchini, Harmonize unaoitwa 'Ushamba' umeibua mjadala mkali katika mitandao ya kijamii, baada ya mmoja wa mtu aliyetumika kupamba video hiyo kufanana na Diamond Platnumz.

Wimbo huo ulianza kutiliwa wasiwasi kabla ya kutoka video yake, kutokana na baadhi ya mashairi kuonekana kama yanamlenga Diamond, na hivyo wengi waliona sawa na dongo la gizani.

Harmonize aliutambulisha wimbo huo kwa aina ya kipekee, baada ya kuandaa pati maalum ambayo waalikwa wake walivaa nguo za ajabu ili kuonyesha wao ni washamba.

Alipoimba kwa mara ya kwanza, baadhi ya mistari ilionekana kumgusa Diamond moja kwa moja, hata hivyo Harmonize mwenyewe pamoja na uongozi wake wamekana hilo, wakisema wimbo huo ni ubunifu wa kisanii tu.

Hata hivyo, video ya wimbo huo ilipotoka rasmi, kile walichohisi watu na kutilia shaka baadhi ya mashairi yake, ilionekana hawakukosea kwani katika video hiyo kuna kipande ambacho kinamuonyesha mtu anayefanana na Diamond, jambo ambalo limezidisha joto kwa mashabiki wa muziki.

Wachambuzi wengi wamesema kuwekwa kipande hicho hakikufanywa kwa makosa, kwani lazima kutakuwa na maana halisi.

"Haiwezekani kuwekwa mtu anayefanana kabisa na Diamond, katika video ya wimbo ule, lazima kutakuwa na jambo fulani na hapo ndipo tunapohisi vita kati ya wanamuziki hawa imeanza rasmi," alisema Kareem Abasi.

Abasi amesema baada ya wimbo "Ushamba" tutarajie jibu kutoka kwa Diamiond Platnumz, ambaye anasifika kwa tabia yake ya kueleza hisia zake kupitia nyimbo hasa pale anapokwazwa au kuchokozwa jambo Fulani.

"Kama Diamond ataendelea na tabia yake ya kutoa dukuduku kwa kutumia nyimbo, basi tutarajie jibu hivi karibuni, na akifanya hivyo mambo yatazidi kuwa mabaya kwa wasanii hawa," ameongeza.

BASI SAWA

# Belle 9 amshukuru Mungu Kiinjili

MWANAMUZIKI nyota wa RnB, Belle 9, amesema ameamua kumrudia Mungu kwa kuimba wimbo wenye mahadhi ya Injili kama tafakari yake baada ya kuponea chupuchupu katika ajali ya gari.

Katika ajali hiyo mbaya iliyohusisha lori na gari dogo yeye na wasanii wenzake Bonge la Nyau na Lulu Diva, Mungu pekee ndiye aliyewanusuru.

Belle 9 amesema eneo ambalo yeye alikaa ilikuwa vigumu kusalimika, lakini amefanikiwa kutoka salama ndiyo maana akaimba wimbo huo wa injili ili kumshukuru Mungu.

Ajali hiyo ilitokea Septemba 7, mwaka huu, katika eneo la Chalinze, wakati wanatoka kwenye kampeni za Chama Cha Mapinduzi (CCM) Ilolo, mkoani Iringa



# Chege bado unamkumbuka Magufuli

VUMBI la uchaguzi mkuu wa kuchagua Rais, wabunge na madiwani, bado lipo kwa mwanamuziki mkongwe wa Bongo Fleva, Chege, kwani bado anakumbuka jinsi Rais, Dk. John Magufuli, walivyosakata muziki pamoja.

Rais Magufuli, alikuwa na matukio ya kipekee kwa wasanii wanaokwenda kutumbuiza katika mikutano yake, ikiwamo kuwapa kofia na kucheza muziki pamoja,.

Akizungumza tukio hilo kupitia kipindi cha PlanetBongo ya East Africa Radio, Chege amesema "Mheshimiwa alihama jukwaa la waheshimiwa akanifuata kumaliza shoo na mimi, wakati Rais ananifuata jukwaani nikazuiliwa ila yeye akasema niachiwe nikacheza naye"



Ameendelea kusema "Nimegundua watu wa siasa wapo mbali na muziki ila wanaupenda,"



# Dogo Janja, Young Dee mambo safii

SASA mkali wa HipHop, Dogo Janja, ameamua kumaliza bifu lake na msanii mwenzake Young Dee, baada ya maneno kuzidi kuhusu ugomvi wao.

Dongo Janja, wiki hii aliamua kushiriki kwa 'EP' ya Young Dee, katika ukurasa wake wa Istagram, huku akimpa heshima zote na kumwita mfalme wa wasanii wote wa kizazi cha sasa.

"Kati ya watu niliokutana nao ambao ni walimu, huyu chalii Youngdaresalama yumo! bonge la EP kamanda, Mfalme wa Young Generation" ameandika Dogo Janja



# Jamani Wema usichanganyikiwe

MWIGIZAJI maarufu wa Bongo Muvi, Wema Sepetu, ameweka wazi kitu ambacho kinaweza kumchanganya na kumfanya aweweseke kwa muda mrefu

Wema Sepetu ameeleza hilo kwenye 'Insta Story' yake baada ya kutoa fursa ya kuulizwa maswali 50 na mashabiki zake, amesema siku akijifungua mtoto anaweza kuchanganyikiwa kwa siku mbili au tatu.

"Naweza kuchanganyikiwa kwa siku mbili au tatu naamini, hata mimi ningependelea hivyo ipo siku inshaalah" amesema Wema wakati akimjibu shabiki wake.

# HUKU KONDA, KULE MUZIKI

**Na Adam Fungamwago**

BONGO imepitia vipindi mbalimbali vya kukumbukwa kwenye masuala ya muziki. Kama tulivyoona huko nyuma kulikuwa na bendi za majeshi ambazo hadi leo zipo, lakini wakati huo zilikuwa na nguvu mno na kutamba, kiasi cha kujizoela mashabiki wengi nchini.

Miaka ya '70 mpaka '90 mwanzoni, Tanzania ilikuwa na bendi za Mashirikika ya Umma, kampuni, mpaka Jumuiya za chama. Mfano Juwata Jazz ilikuwa ikimilikiwa na Jumuiya ya Wafanyakazi chini ya Chama cha Mapinduzi  na Vijana Jazz ilikuwa ikimilikiwa na Jumuiya ya Vijana ya Chama cha Mapinduzi.

Leo tunaziangalia bendi zilizokuwa zikimilikiwa na Mashirikika ya Umma. Ni kwamba bendi hizo zilikuwa na baadhi ya wanamuziki ambao walikuwa ni wafanyakazi wa mashirika hayo. Ni wachache tu ndiyo walikuwa wanapiga muziki tu.

Wanamuziki waliokuwa na vipaji vya kazi zingine, kusomea au uwezo, walipewa kazi kwenye mashirika hayo, huku wakipiga muziki.

**UDA Jazz Band 'Bayankata'**

Vuta picha konda na dereva wa daladala au mabasi ya UDAT unayoyaona leo, wakimaliza kazi zao za kutwa nzima watoke hapo kwenda kupiga muziki. Na siku zingine wanakwenda kwenye mazoezi, wakimaliza wanaingia mzigoni kuendesha mabasi na kutoza nauli abiria kama kawaida.

Ndivyo ilikuwa kwa bendi ya Uda Jazz. Ilikuwa na wanamuziki wengi ambao ni madereva wa mabasi ya abiria, makonda, mafundi gereji, mafundi wa taa za magari na mengineyo.

Mfano mtunzi wa vibao vya 'Tulele Tuboe' na 'Nenda Kaishi Salama', Mikidadi Seif ambaye alifariki katikati ya mwaka huu, alikuwa ni kondakta wa mabasi ya UDA. Hamza Kalala yeye alikuwa fundi ya taa za magari.

Ilikuwa ni bendi maarufu sana nchini na kurekodi nyimbo nyingi zilizopenda kama hizo zilizotajwa hapo juu. Zingine ni 'Nachunga Heshima' na 'Sakina Kaharibu Masomo'.

**National Panasonic Band**

Hii ilikuwa ni bendi ya kiwanda cha kutengeneza redio pamoja na betri maeneo ya barabara ya Pugu jijini Dar es Salaam.

Haikuwa maarufu sana, na haikudumu muda mrefu sana, lakini ilikusanya wanamuziki mahiri na kutoa baadhi ya vibao vilivyotamba sana.

Vibao kama 'Fahari ya Macho' na 'Tofiki' ambavyo vilitesa sana kwenye anga la muziki wa dansi hadi leo hii.

**Biashara Jazz Band**

Ni bendi iliyokuwa inamilikuwa na Kampuni ya Biashara za Ndani. Ilikuwa ikiongozwa na Juma Ubao maarufu kama 'King Makusa'.

Nayo pia haikuwa maarufu sana kwa jina, kuliko hata kiongozi wa bendi hiyo, King Makusa ambaye alikuwa maarufu zaidi. Nyimbo maarufu zaidi za bendi hiyo ni 'Posa Nitaleta', 'Kipini cha Dhahabu', na nyingine nyingi.

**Bima Lee 'Magnet Tingisha'**

Shirika La Bima la Taifa ndilo lilikuwa likiimiliki bendi hii na haikuwa bendi ya muziki tu, bali hata kundi la taarabu.



Ilikuwa ni moja kati ya bendi kubwa kabisa nchini, iliyozitikisa bendi kubwa kama Msondo Ngoma na Sikinde Ngoma ya Ukae.

Iliweza kuchukua wanamuziki kadhaa kutoka Sikinde kama Joseph Mulenga, Abdallah Gama, Suleiman Mwanyiro, Shaaban Dede na wengineo. Ni bendi iliyokuwa na nyimbo nyingi sana maarufu kama 'Makulata', 'Baba Shani' na nyinginezo.

**Tancut Almasi Orchestra**

Awali ilisemekana kuwa ni bendi iliyokuwa ikimilikiwa na kiwanda cha kukata almasi mkoani Iringa, lakini baadaye ilikuja kubainika kuwa bendi hiyo ilikuwa ikimilikiwa na wafanyakazi wa kampuni huyo kama wao na si kampuni yenyewe ya kuchonga na kukata almasi.

Ni moja kati ya bendi kubwa zilizotikisa nchini Tanzania, na wimbo wake maarufu zaidi ni 'Masafa Marefu.'

# Mchawi wa Kijiji: Ulimi uliponza kichwa

**Na Adam Fungamwango**

UCHAWI ni dhana ya kufikirika iliyojengeka hasa kwenye nchi za Kiafrika. Ni dhana ambayo baadhi ya watu huamini kuna binadamu wana nguvu za ziada ya kufanya mambo ambayo hayawezi kufanyika kwa biandamu wa kawaida. Inadhaniwa kuwa mchawi anaweza kumuua binadamu kwa njia za mazingara na si kumpiga au kumchoma na kitu chochote kile.

Inaaminika kuwa mchawi huwezi kumtesa bindamu wa kawaida kwa magonjwa ambayo hayawezi kuonekana kwa vipimo vya kawaida akienda hospitalini, labda kwa mganga wa kienyeji.

Pia inadaiwa mchawi ana uwezo wa kumtia mtu mikosi na kushindwa kupata kazi, kuolewa, kuoa au kufanya kitu chochote kile kikafanikiwa.

Leo tuna filamu iitwayo 'Mchawi wa Kijiji' ambayo inahusiana na dhana hiyo.

Mara nyingi ulimi ni kiungo kidogo sana, lakini kina uwezo wa kusababisha jambo likawa kubwa na kuleta uhasama na maafa sehemu yoyote ile.

Mzee Makoti ambaye ni maarufu sana kijijini kutokana na tabia yake ya kupenda kutembea na wake za watu, pamoja



na mabinti, anapita kwenye moja za njia kijijini.

Anakutana na mabinti ambaye wanamsimamisha na kumwambia aache tabia yake mbaya.

Kiswaswadu, binti mwenye uwezo mkubwa wa kuongea kama kameza kanda au CD, anamchana mzee huyo aache tabia yake huyo.

Mzee Makoto anamuonyeshea kidole na kumwambia kwa sababu yeye ndiye ameongoza kundi la mabinti hao kumsema yeye, basi hatoliona tena jua la kesho.

Jioni yake Kiswaswadu anagongwa na bodaboda na kufariki dunia. Shoga zake wanatambua kuwa hiyo ni kazi ya mzee Makoti ambaye aliongea maneno ya kumtisha shoga yao.

Habari zinaenea kijijini kuwa mzee Makoti ndiye aliyemuua Kiswaswadu. Mzee anaanza kuogopeka na kutengwa.

Hii inamtia simanzi mno mzee wa watu, kwani ukweli ulio moyoni mwake ni kwamba si mchawi, ila aliongea tu maneno hayo kwa hasira. Lakini nani atamuamini wakati aliposema tu, binti wa watu akafa kweli kwa ajali ya bodaboda?

Akili yake ikamtuma sasa ajifanye mchawi kweli ili wazidi kumuogopa. Akawa anavaa sasa matunguli na kutembea nayo. Hii ilizidi kuwatisha wanakijiji.

Mzee Makoti akawa anatumia faida ya kuogopwa, kutembea na vibinti kidogo kila anapokutana navyo njiani porini.

Aliwamaliza karibu mabinti wote kijijini, kutokana na vitisho kuwa wakimkatalia atawageuza nzi, wengine paka, mbwa na wanyama wengine.

Mwisho wa siku wanakijiji wanaamua kwa kauli moja kuacha woga na kumkamata na kumuonyesha kazi.

Na kweli wanakusanyika na kumkamata, wanampa msukosuko wa maana, mpaka mwenyewe anaamua kueleza ukweli wote kuwa yeye si mchawi, ila alikuwa ameamua kufanya hivyo ili watu wamhofie. Na hii ni baada ya tukio la kumuonyesha mtu kidole na kutisha, baadaye akafa kweli.



# Simi avunjika moyo kwa hili...

MWANAMUZIKI maarufu wa kike kutoka Nigeria, Simi, amekuwa na hofu kutokana na kuendelea kwa vitendo vya unyanyasaji wa kijinsia dhidi ya wanawake nchini humo.

Katika ujumbe wake aliouweka katika ukurasa wake wa Twitter, Simi, kila kukicha anakuwa na hofu na moyo wake unavunjika kutokana na taarifa mbaya zinazowahusu wanawake.

"Wanawake wanapata shida, kila siku moyo unavunjka kutokana na matukio ovu wanayofanya wanawake ambao ni dhaifu na hawana nguvu za kujitetea," amesema Simi.



## Rahama hajui jela kulivyo

MWIGIZAJI nyota kutoka Kannywood, Rahama Sadau, amepuuza taarifa kwamba alikamatwa na kufungwa jela.

Katika ujumbe wake kupitia ukurasa wa Twitter, Rahama, amesema hakuwahi kuitwa na polisi wala kufikishwa katika mahakama yoyote kujibu mashtaka.


"Nimepokea ujumbe mwingi kwamba nimekamatwa na kuhukumiwa jela. Sijui habari hiyo ilitoka wapi. Kwa hivyo natoa mwito kwa watu kuacha kueneza taarifa feki," amesema.

## Lil Frosh sasa yatakukuta shauri yako

RAPA kutoka Nigeria, Sanni Goriola, maarufu kama Lil Frosh, amemjeruhi tena mpenzi wake Gift Camille, baada ya kumshushia kipigo kikali.

Hata hivyo, katika mahojiano ya hivi karibuni, Lil Frosh, amekanusha akisema hakumpiga mpenzi wake huyo, badala yake inawezekana ana tatizo la mzio linamsumbua.

"Sikufanya jambo hilo, huyu ni mpenzi wangu, yawezekana ana matatizo ya mzio unamsumbua na ndio maana amevimba," amesema Frosh.





## Alipotoka, anapokwenda Tiwa Savage

MSANII mkongwe wa muziki wa Nigeria, Tiwa Savage, amesimulia safari yake ya kimuziki, akisema ilikuwa na mabonde mengi kiasi kwamba alikata tamaa.

Alisema wakati anachipukia, lebo kubwa za muziki zilikataa kufanya kazi, na hatimaye aliangukia mikononi mwa meneja wake wa zamani Teebillz.


Alisema katika kukamilisha ndoto zake, aliamua kwenda katika lebo ya Mavn iliyo chini ya Don Jazzy, baada ya kugundua inafanya kazi vizuri.

## Uchemba usiishie uchumba tu

MWIGIZAJI maarufu wa filamu za watoto kutoka Nollywood, Williams Uchemba, amemchumbia mpenzi wake wa muda mrefu, Brunella Oscar.

Staa huyo alitoa taarifa kupitia ukurasa wake wa Istagram, akisema kuna wakati kila mwanamume anahitaji kuwa karibu na mwanamke anayempenda.

"Hoja yangu kuu ni kumshukuru Mungu kunipa mwenzi wangu wa maisha ambaye anaweza kuelewa," ameandika Uchemba.



MAKALA

# JERRY JOHN RAWLINGS

## ■Mwanajeshi aliyepindua serikali mara mbili
## ■Ameiacha Ghana nchi ya asali na maziwa

**Mwandishi Wetu**

BARA la afrika limeondokewa na kiongozi wake mashuhuri, Rais wa zamani wa Ghana, Jerry Rawlings, ambaye alifariki Dunia siku ya Alhamisi ya wiki hii akiwa na umri wa miaka 73.

Rawlings atakumbukwa kama kiongozi aliyetoa mchango katika bara la Afrika, kutokana na uongozi wake imara uliokuwa ukiegemea kuwajali watu maskini.

Kabla ya kuingia madarakani, Rawlings, aliongoza mapinduzi ya kijeshi nchini Ghana mara mbili na baadaye kuleta mfumo wa demokrasia kwa taifa hilo la Afrika Magharibi.

Katika mapinduzi ya kwanza, akiwa na cheo cha luteni, alimng'oa madarakani, aliyekuwa Rais wa nchi hiyo, jenerali Fredrick Akuffo, mwaka wa 1979.

Baada ya kuipindua serikali, aliamua kukabidhi madaraka kwa serikali ya kidemokrasia, lakini miaka miwili baadaye, akaongoza tena mapinduzi ya pili ya kijeshi, akishutumu serikali hiyo kuwa ya ufisadi na uongozi dhaifu.



Jerry Rawlings, alikuwa na tabia ya kushangaza na ni vigumu kutokea kwa viongozi wengine wa Kiafrika. Kabla ya kuamua kuongoza Ghana, Rawlings, aliangusha serikali mara mbili, lakini hakutaka kuongoza na badala yake aliwakabidhi watu wengine kuongoza kwa njia ya kidemokrasia .

Miaka miwili baadaye Rawlings, alimuondoa madarakani kiongozi wa nchi aliyechaguliwa kidemokrasia kasha alifanikiwa kugombea mwenyewe katika uchaguzi.

Awali Rawlings ambaye anafuata siasa za kijamaa, alianzisha sera ya mageuzi ya soko huria na kuifanya nchi yake kuwa ya mfano kimataifa.

**JERRY RAWLINGS NI NANI?**

Jerry John Rawlings, alizaliwa katika mji wa Accra Juni 22, mwaka 1947, akiwa mtoto wa kiume wa baba mkulima kutoka Uskoch, nchini Uingereza na mama raia wa Ghana.

Elimu yake ya msingi na sekondari alisomea katika shule ya sekondari ya Achimota, huko alifanya vizuri kielimu na pia alijifunza mashindano ya mbio ya farasi.

Watu waliosoma pamoja, wanasema Rawlings, alikuwa na kipaji kikubwa cha kuongea na hakuwa muoga kuelezea maoni yake hata kama yalionyesha uasi.

Mwaka 1968, alijiunga na shule ya mafunzo ya kijeshi ya Teshie, karibu na mji mkuu wa Accra, na baadaye alipelekwa katika shule ya uendeshaji wa ndege.

Akiwa na cheo cha Luteni, alipata bahati ya kujiunga katika kikosi cha askari wasomi (Fourth Squadron) ambacho kinahusika na undeshaji wa ndege za kijeshi.

Wakati Rawlings alipopandishwa cheo kuwa Luteni mwaka 1978, alikuwa tayari ameanza siasa.

Ghana, ambayo ilikuwa nchi ya kwanza Afrika kupata uhuru wake kutoka kwa Uingereza, ilikuwa inakabiliwa na tatizo la uhaba wa chakula na mkwamo wa kiuchumi.

Kila mara Rawlings alionyesha hasira zake kwa kile alichokisema serikali zilizokosa nidhamu, ufisadi na matumizi mabaya ya utawala wa kijeshi.

Baada ya kuruhusiwa kwa mfumo wa vyama vingi vya siasa mwaka 1979, Rawlings alipata umaarufu mkubwa kutokana na ukosoaji wake wa serikali. Aliitaka ifanye juhudi kuwasaidia masikini. Akisukumwa na uungaji mkono wa raia, Rawlings alifanya jaribio lake la mapinduzi, Mei mwaka 1979. Katika jaribio hilo ambalo halikufanikiwa, alikamatwa na kuhukumiwa kifo.

Hata hivyo, alifanikiwa kutoroka jela baada ya kupata msaada kutoka kwa maofisa wa ngazi ya chini na vyeo vingine.

Baada ya kurudi uraiani, alifanikiwa kumpindua kiongozi wa kijeshi wa nchi hiyo, Jenerali Fred Akuffo. Rawlings alichukua utawala chini ya Baraza la kijeshi la mapinduzi (AFRC).

AFRC iliapa kuwawajibisha viongozi wa zamani, na Akuffo na viongozi wengine wa kijeshi walinyongwa.

Rawlings alianzisha sera mpya ya kuinua nchi kiuchumi na kuita kama 'Housekeeping exercise' ambayo ililenga kuiondoa Ghana katika kile AFRC walichokiamini vitendo vya ufisadi wa utawala wa kijeshi.

Majaji wa ngazi ya juu kadhaa na maofisa wa jeshi waliuawa katika kipindi hicho.

Lakini, mbali na kung'ang'ania madaraka mapya aliyoyapata, Rawlings aliitisha uchaguzi katika kipindi cha miezi minne ya mapinduzi yake.

Chama kipya cha People's National Party, kilichoongozwa na Hilla Limann, kilipata ushindi na kukabidhiwa madaraka.

Hata hivyo, Limann alionekana na wengi kama mtu anayetumiwa na Rawlings, na kushindwa kwake kufanya mageuzi ya uchumi kulimfanya aondoke madarakani haraka.

Wakati anaondoka, nchi hiyo ilikuwa ikikabiliwa na matatizo mengi ikiwamo kuongezeka kwa madeni na mfumuko wa bei kuwa asilimia 140, jambo liloibua ghadhabu na machafuko.

Ilipofika Desemba 31, mwaka 1981, Rawlings aliingilia kati kwa mara ya pili, akafanya mapinduzi ambayo yaliiweka madarakani serikali mpya iliyo chini ya baraza la kijeshi liloitwa ' Provisional National Defence Council (PNDC).

PNDC, kikiongozwa na Rawlings kilitaka kuibadili Ghana kufuata siasa za kijamaa.

Rawlings aligeukia muungano wa Usovieti kuomba msaada, lakini baada ya miaka miwili tu katika jaribio lake kwenye ujamaa, Ghana iliuacha na kuafuata sera ya soko huria ambayo inakumbatiwa na nchi za Magharibi.

Katika utawala wake, alishusha thamani ya sarafu, akaacha kuwaajiri wafanyakazi katika kampuni ya serikali na kutaifisha viwanda.

KUPATA USHINDI

Lakini, ingawa mabadiliko haya yalizifurahisha nchi za magharibi pamoja na Mfuko wa fedha duniani(IMF), makali yaliyoambatana na mageuzi hayo yalisababisha machafuko ndani ya nchi.


Kati ya mwaka 1983 na 1987, Rawlings alinusurika kupinduliwa katika majaribio manne dhidi yake. Serikali yake ilendesha zoezi la kamatakamata kwa wanasiasa wa upinzani ambao wengi walifungwa.

Lakini, kufikia miaka ya 1990, mageuzi yake yaliongoza nchi hiyo katika mafanikio ya kiuchumi. Mwaka 1992, Rawlings akashinda uchaguzi wa rais.O CHA PICHA,GETTY IMAGES

Ushindi wake wa asilimia 58% ya kura, ulielezwa na waangalizi wa Kiamataifa kuwa ulikuwa wa haki. Kutokana uchumi imara, kiongozi huyo alichaguliwa tena mwaka 1996.

Katika utawala wake, sura ya Ghana iling'aa kimataifa na kuaminiwa katika vikosi vya kuleta amani vya Umoja wa Mataifa. Askari wake walipelekwa kulinda amani katika nchi za Liberia, Sierra Leone, Lebanon na Iraq.

**Kwa msaada wa BBC**





# Mhitimu udaktari, mwanafunzi bora wa Kemia kitaifa aibua siri

## ■Awaonyesha waliobaki pa kupita
## ■Alikosoma; apewa chaki, jina mtaa
## ■Mzazi & mwalimu; tabasamu acha!

**Na Martha Willy**

NI desturi kila yanapotoka matokeo ya mwisho kuanzia darasa la saba hadi kidato cha sita kutangazwa wanafunzi 'kumi bora' kitaifa.

Wengi hujiuliza, wako wapi wale bora wa siku zilizopita, wanafanya nini na je bado ni bora?

Ni swali ambalo Nipashe iliifunga safari hadi katika Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS) na kukutana na Aliko Mwakyembe, mhitimu wa fani ya udaktari hivi karibuni, aliyeng'ara mwanafuzi bora kitaifa wa somo Kemia, kidayo cha sita mwaka 2016.

Anasema historia na mafanikio hayo ni zao la mambo kadhaa. Mazungumzo ya 'ana kwa ana' na Nipashe yalikuwa namna hii:

**SWALI:** Naomba kujua maisha yako shuleni?

**JIBU:** Mimi kwa kawaida napenda sana kutumia muda wangu kujisomea na kudadisi kwa kina mambo yote ambayo ni magumu kwangu.

**SWALI:** Unadhani kwanini ulifaulu somo la Kemia na kuibuka kinara kitaifa?

Aliko: Ni somo ninalolipenda sana tangu 'O-Level' (kidato cha nne), pia walimu waliokuwa wananifundisha walikuwa kama marafiki kwangu, hivyo nilijitahidi nisifeli maana niliogopa nitapata aibu, aibu kwao maana waliniweka karibu sana.

Nakumbuka mara ya kwanza nilipokuwa kidato cha tano, kuna mtihani tulifanya swali moja nilipata peke yangu. Tangu siku hiyo mwalimu akaniita na akaniambia kwamba endapo nitafeli basi nitashughulikiwa.

Tangu hapo nikaweka uzito kwenye somo la Kemia. Kwa kuwa nilipenda, ilikuwa rahisi sana kulisoma na kulielewa. Nilitumia muda mwingi 'ku-solve' (kujibu) maswali mbalimbali na hii ilinisaidia sana, kwa kuwa na uwezo wa kujibu mtihani chini ya wakati uliopangwa.

Mtihani wa Taifa wa takribani saa mbili za kwanza, muda uliobaki niliutumia kuhakiki.

**SWALI:** Ilikuwaje ulifanya mtihani mapema na kwa usahihi?

JIBU: Maswali mengi yalifanana na yale niliyokua napenda kuyapitia mara kwa mara nilipokuwa na muda wangu wa ziada, hivyo ilikuwa rahisi sana kwangu kukumbuka jinsi ya kufanya maswali hayo, lakini hata kwa yale ambayo yalikuwa mageni, kwa kuwa nilifanya maswali mengi kabla ya mtihani wa mwisho.

Niliweza kuwa na akiba ya mawazo ambayo yalinisaidia kujibu. Pia, baadhi ya maswali yalikuwa kwenye vitabu ambavyo nilikuwa navitumia mara kwa mara.

Hivyo, mengine sio kwamba nilikumbuka njia pekee, bali hadi majibu ya maswali hayo nilikumbuka.

**SWALI:** Unataka kuniambia kwamba ukaribu wako na walimu na kukufanya rafiki kulichangia ufaulu wako wa kiwango cha juu na kukuibua kama kinara wa somo la Kemia kitaifa?

**JIBU:** Hii ni moja kati ya sababu kwa upande wangu, lakini zaidi ni zile juhudi nilizoweka kwenye somo husika.

**SWALI:** Je, unawaambia nini wanafunzi wanaodhani ni ngumu kupata tuzo za kitaifa na labda zinatolewa kwa watu fulani?

**JIBU:** Dhana hiyo ni potofu, kwa maana kama ingekuwa inatolewa kwa watu fulani, basi pasi na shaka wangekuwa wanapata watu fulani waliosoma shule zenye majina makubwa.

Sio kweli, kwa kuwa mimi kuanzia shule ya awali na kidato cha nne nimesoma shule za serikali wanazoziita 'shule za Kayumba' lakini nilifanikiwa kupata tuzo hiyo.

**SWALI:** Je ufaulu wako katika masomo yako ya utabibu, unashabiliana na tuzo uliyopata?

**JIBU:** Kwa wakati huu ni vigumu kukiri hicho, lakini nilielekeza jitihada zangu katika masomo hivyo naamini hata ufaulu wangu utashabiliana na tuzo niliyopata toka kwa Mkemia Mkuu wa Serikali Mstaafu, Profesa Samwel Manyere.

**SWALI:** Una ushauri gani kwa wanafunzi wanaotamani kuibuka vinara kitaifa katika masomo mbalimbali?

**JIBU:** Wanatakiwa kwanza walipende somo, maana hapo ndipo watawaeza kulipa muda wa kutosha, pia itarahisisha uelewa.

Kingine, wakati wa likizo kutumia muda mwingi kujisomea na kuunda vikundi vya kusaidiana kutokana na uelewa tofauti, ili kupata mwanga wa yale ambayo yapo kwenye somo husika .

### MWALIMU WAKE

Nipashe ilihamishia udadisi kwa Mwalimu wa Kemia kutoka shule ya Sekondari ya Wazazi wa Pandahill, Salim Khamis, kuhusu mwanafunzi wake bora, naye hakusita kumtambua kwamba alijituma sana.

Anasema, alifikia hatua mwalimu alipopatwa na dharura, Aliko alikabidhiwa darasa kuwafundisha wenzake, hata mwalimu alipowadadisi baadaye, aliwakuta wanaelewa na wanafurahia ufundishaji wake

Pia, anamtaja kuwa msikivu na mwenye nidhamu, mdadisi anayetaka kuelewa kila mara, jambo lililochangia ufaulu wake.

Kwa sasa, anasema amekuwa msaada kwa wanafunzi katika kipindi chote cha likizo zake kutoka chuoni MUHAS, ametumia kuwafundisha na kuwasaidia wanafunzi wa shule yake ya Pandahil, somo la Kemia.

"Pia nilijisikia msisimko, pale nilipopata taarifa kutoka kwa Mkuu wa Shule kwamba natakiwa nikapokee tuzo yangu kutoka kwa Mkemia Mkuu Mstaafu wa Serikali, Profesa Samwel Manyere, kama mwalimu niliyekuwa nikimfundisha mwanafunzi kinara wa somo la Kemia kitaifa ndugu Aliko Mwakyembe. " Kwa kweli, ingawa aliipa shule heshima kubwa, lakini hata mimi pia nilipata heshima, maana nilikuwa na furaha kubwa kwa mwanafunzi wangu kunitambulisha mimi mwalimu wake kitaifa," anasema Mwalimu Khamis, anayeongeza:

"Tulipoona kwamba ana moyo wa kujitolea kufundisha wenzake, ndio sababu ambayo ilitufanya tumuombe awe anakuja kuwasaidia



Mhitimu wa udaktari wa Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS) akitunukiwa shahada.

wanafunzi wenzake pale anapokuwa likizo, ili awape changamoto wanafunzi wenzake, kwa kuwa wanafunzi wengi wanatamani siku moja kuwa kama yeye... ni mwanafunzi myenyekevu na mwenye heshima kwa kila mtu".

Anataja heshima mojawapo waliotoa kutambua mchango wake, ni kumpatia heshima, moja ya vibao vya ya shule, inaitwa 'Aliko Mwakyembe Street.'

### KUTOKA FAMILIA

Mama yake mzazi, Sara Kasumo, naye alikuwa na ufafanuzi wenye marejeo: "Aliko ni mtoto msikivu wa kiwango cha juu na mtoto ambaye anapenda sana kutumia muda wake kubuni vitu. Anapenda sana kusoma na ni mpigaji mzuri wa kinanda kanisani."

Pia, anamtaja hana tabia ya ulimbukeni ya kupotoshwa, hapendi magenge, vijiwe vya soga na mwenye upendo kwa wenziwe.

Aliko anawataka wanafunzi wanapokuwa shuleni kipaumbele chao kiwe masomo, kwani kila kitu mtu akikipenda, kupigania na kuweka kando yasiyo ya umri wao, ndoto ya kijana inapatikana.

Anadokeza uzoefu wa wanafunzi wengi shuleni wana maisha ya kuiga na matokeo yake wanajiingiza katika hatari za kukatisha ndoto zao, akitaja mifano ya uvutaji bangi na uhusiano wa kimapenzi.

"Mimi nilisikiliza sana wosia wa wazazi wangu na kwa kuwa nawapenda, sikupenda siku moja niwaumize na kuwasononesha na kuona ile juhudi yao waliyotumia kunisomesha na kunilea igeuke kuwa maumivu na majuto katika maisha yao.

"Mimi ninavyoelewa, kila mzazi furaha yake ni kuona mwanawe anapiga hatua nzuri katika maisha, hivyo nadhani hadi sasa nimeongeza siku za wazazi za kuishi, maana kitaalamu moyo ukichangamka hata siku za kuishi.

Aliko alizaliwa Novemba 5, mwaka 1995 mjini Mkoani, akiwa mtoto wa pili katika familia ya watoto wanne ya baba Nicholous Mwakyembe na Sara Kasumo.

Alimaliza elimu yake ya awali na kisha msingi katika shule ya Mwakibete mjini Mbeya na alihitimu kidato cha nne katika shule ya sekondari Mbeya Day mjini hapo.

Baadaye aliendelea na kidato cha tano na sita, Shule ya Sekondari ya Pandahill wilaya ya Songwe, Mbeya, alikoibuka kinara wa Kemia kitaifa.

# Iran yaongeza kasi urutubishaji nyuklia

**NEWYORK, Marekani**

NCHI ya Iran sasa imeongeza kiwango chake cha urutubishaji wa madini ya Uraniaum mara 12, kinyume na mkataba wa nyuklia wa mwaka 2015.

Taarifa hiyo mpya iliyotolewa na Shirika la Udhibiti wa Nyuklia Duniani (IAEA), imezusha wasiwasi kwa nchi jirani za ghuba.

Shirika hilo lilisema kuwa akiba ya uranium imefikia kiwango cha chini cha kilo 2,442.9 hadi mwezi huu.

Hata hivyo, Iran inasisitiza mipango yake ya nyuklia ni kwa ajili ya amani na si vinginevyo.

Kwenye taarifa hiyo, ilisema kuwa maelezo ya Iran kwa ajili ya uwepo wa nyuklia hiyo katika eneo ambalo halijaliwekwa wazi sio ya kuaminika.

Kwenye ujumbe wa Twitter, balozi wa Iran katika IAEA, Gharib Abadi, alisema kuwa kauli zozote za haraka zinapaswa kuepukwa.

"Mazungumzo yanaendelea kwa lengo la kukamilisha azimio la suala hilo ." alisema.

Chanzo ambacho hakikutajwa kililiambia shirika la habari la AFP, kwamba, vifaa vilivyopatikana havikuonyesha kiashiria chochote kwamba havikutumiwa katika urutubishaji wa uranium, lakini inawezakana vilitumiwa kutunza nyuklia.

IAEA liliongeza kuwa Iran inaendelea kurutubisha uranium kutakatisha hadi kufikia kiwango cha asilimia 4.5, na huo ni sawa na ukiukwji wa asilimia 3.67 ya makubaliano katika mkataba wa mwaka 2015.

Shirika hilo bado linachunguza sampuli zilizochukuliwa mwezi Septemba kutoka katika maeneo ya awali yaliyoshukiwa kuwa ni ya nyuklia, ambayo yalifunguliwa kwa ajili ya ukaguzi wa mwaka huu.

Mwaka jana, Iran ilitangaza hadharani kukiuka ahadi zake chini ya mkataba wa kimataifa wa nyuklia uliosainiwa na China, Ufaransa ,Ujerumani, Urusi, Uingereza na Marekani .

Hatua hiyo ilichukuliwa katika kujibu mapigo, baada ya Rais wa Marekani Donald Trump, kuiondoa nchi yake katika mkataba huo na kurejesha vikwazo vya kiuchumi dhidi yake.

Chini ya makubaliano hayo, Iran iliruhusiwa uzalisha kilo 300 za uranium katika eneo maalumu ambalo ni sawa na kilo 202.8 za uranium.

Muda mfupi baada ya kutolewa kwa ripoti ya IAEA , Mfalme Salman wa Saudi Arabia, ambaye ni hasimu wa Iran katika kanda hiyo, alisema dunia inapaswa kuidhinisha msimamo ili kuhakikisha nchi hiyo haipati silaha za maangamizi.

"Ufalme unasisitiza hatari za mradi wa Iran kwa kanda , uingiliaji wake katika nchi nyingine, unachochea ugaidi, inawasha moto ya kidhehebu. Miito ya msimamo kutoka kwa jamii ya kimataifa dhidi ya Iran inadhihirisha jinsi inavyoshugulikia juhudi zake za kupata silaha za maangamizi na kutengeneza mpango wake wa makombora yake," alisema.

Rais mteule wa Marekani, Joe Biden, ameashiria utashi wa Marekani wa kujiunga na mkataba wa nyuklia, na kuipa Iran njia nzuri ya kurejea katika diplomasia.

Kiongozi wa Iran, Hassan Rouhani, alijitetea kwa kusema nchi yake itatumia fursa yoyote kuondoa shinikizo la vikwazo kutoka kwa watu wake.

*BBC*



Wanamgambo wa Tigray wakiwa nje makao makuu ya jimbo hilo, kujilinda dhidi ya askari wa Ethiopia. **(PICHA: BBC)**

# kiongozi mpya Tigray apatikana

**ADIS ABABA**

BUNGE la Ethiopia, jana limemchagua kiongozi mpya wa Mkoa wa Tigray, wakati vikosi vya serikali kuu vikizidisha mashambulizi ya kijeshi dhidi ya wanamgambo wa eneo hilo.

Tangazo hilo lilitolewa na Waziri Mkuu Abey Ahmed, siku chache baada ya chombo hicho kumwondolea kinga ya kushtakiwa kiongozi wa Tigray, Debretsion Gebremichae, ambaye alichaguliwa Septemba mwaka huu.

Wakati hali ikiendelea kuwa mbaya katika jimbo hilo, Umoja wa Mataifa umeitaka Ethiopia kutoa nafasi ya kupatikana msaada wa kiutu kwenye Mkoa wa Tigray na kuruhusu raia kuondoka kwa usalama.

Pia imeitaka serikali kuhakikisha ulinzi kwa wafanyakazi wa huduma za msaada.

Zaidi ya watu 11,000 ,wamekimbia na kuingia nchi jirani ya Sudan tangu serikali ya shirikisho alipoanzisha operesheni ya kijeshi dhidi ya chama kinachoongoza mkoa huo cha TPLF, mwanzoni mwa mwezi Novemba.

*DW*

## China yampongeza Biden kushinda ushaguzi

**BEIJING, China**

CHINA imeungana na nchi nyingine duniani kutuma salamu za pongezi kwa rais mteule wa Marekani, Joe Biden.

Pongezi hizo zimekuja wiki moja tangu Biden alipotangazwa na vyombo vya habari vya kitaifa, kuwa mshindi wa uchaguzi wa rais uliofanyika Novemba 3, mwaka huu.

Msemaji wa wizara ya mambo ya kigeni ya China, Wang Wenbin, alisema serikali inampongeza Biden pamoja na Harris Kamala kwa ushindi walioopata, lakini inatambua uamuzi kamili wa uchaguzi wa Marekani utaamuliwa na sheria za taifa hilo.

China ilikuwa sehemu ya mataifa makubwa duniani ikiwamo Urusi ambayo yalijizuia kutoa pongezi kwa Biden kutokana na mvutano unaoendelea juu ya matokeo, baada ya Rais Donald Trump, kukataa matokeo akidai kuibiwa kura.

*DW*

## Watu 74 wafa maji Libya

**TRIPOLI, Libya**

WAHAMIAJI 74 wamekufariki dunia baada ya boti waliyokuwa wakitumia kusafiri wakijaribu kuingia Ulaya, kuzama baharini nje kidogo ya pwani ya Libya.

Shirika la Uhamiaji laUmoja wa Mataifa, (IOM) lilisema boti hiyo ilikuwa imewabeba watu 120, wakiwamo wanawake na watoto wakati ilipozama karibu na bandari ya al-Khums .

Katika ajali hiyo watu 47 pekee ndiyo wameokolewa. IOM ilisema hadi kufikia jana milii ya watu 31 pilipatikana na kuopolewa majini, huku shughuli za kutafuta miili ya watu wengine bado inaendelea.

Tangu kuuawa kwa kiongozi wa muda mrefu wa Libya, Muammar Ghaddafi, nchi hiyo imegeuka kuwa sehemu wanayotumia wahamiaji kutoka Afrika na mashariki ya kati wanaojaribu kuingia nchi za Ulaya.

Mara kadhaa walanguzi hutumia boti za mpira zilizojaa kupita kiasi kuwasafirisha watu kuvuka bahari ya Mediterania.

*DW.*

**Katika ajali hiyo watu 47 pekee ndiyo wameokolewa. IOM ilisema hadi kufikia jana milii ya watu 31 pilipatikana na kuopolewa majini, huku shughuli za kutafuta miili ya watu wengine bado inaendelea.**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## VIWANJA NA MASHAMBA

**NYUMBA INAUZWA IKO KAHAMA** MAJENGO VYUMBA VITATU INA MAJI NA UMEME, PLOT No 759, BLOCK "E", KIWANJA NI MEDIUM SIZE. MAWASILIANO ZAIDI; 0759359933/0713553819

**NIPASHE NI JIBU LAKO**
**NJOO UTANGAZE NASI**
**KWA BEI NAFUU SANA**
Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676

## KUPOTEA KWA CHETI



115997302

**JUSTIN JANUARY MAKUNDI** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.1697/0048** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia NYUMBU SEKONDARI mwaka 2007. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **DAR/CHA/RB/794859/2020.**

## KUPOTEA KWA VYETI



115997402

**EUNICE PAULO PALLANGYO** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.4150/0018/2016** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **NOMELLA SEKONDARI** mwaka 2016. Cheti cha kidato cha nne chenye namba **VTC P.4352/0015/2017** kilichotolewa na MSHIKAMANO VTC mwaka 2017. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/KIL/RB/365316/2019.**

## KUPOTEA KWA CHETI



115997502

**IBRAHIMU METHOD MAFUMIKO** anatangaza kupotea kwa cheti cha DIPLOMA chenye namba **DRM17/09/D.5719** kilichotolewa na **TANZANIA PUBLIC SERVICE COLLEGE (TPSC)** mwaka 2020. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **DAR/RB/5520/2020.**

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI YA 2)**

Katika mahakama ya mwanzo DODOMA MJINI
Usimamizi wa mirathi NA./73/2020

Ombi la **WILLIAM PATRICK MDINDILE** kuteuliwa
Msimamizi wa mirathi Marehemu **ANTONI STEPHEN KIPONDA**
KWA YEYOTE ANAYEHUSIKA TANZANIA BARA
Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo **Tarehe 19/11/2020** kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo.
Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa.
**Tarehe 13/11/2020**

## NDABAKA SAFARI LODGE COMPANY LIMITED

### BOARD RESOLUTION

**SHAREHOLDERS' RESOLUTION APPROVING DISSOLUTION OF THE COMPANY**

Name of the company.... **NDABAKA SAFARI LODGE COMPANY LIMITED**
Registered Address.... **P o Box 541 MWANZA**

At the meeting of the directors held at 10;00 am on 30/12/2006 the following resolution was passed.
The shareholder of the company hereby dissolve the company shall wind up its from 22nd January 2007.

**NOW THEREFORE BE IT RESOLVED** that the company shall wind up its affairs , and the company shall be dissolved.

Dated this ...
Signature: ... Signature: ...
Name: ... Chairman of the meeting/Director Name: ... Company Secretary

**JAMHURI YA MUUNGANGO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455.
Fax: +255 26 2323233.
Barua Pepe: ps@mow.go.TZ.
Tovuti: www.mwtc.go.TZ.

Mtaa wa Moshi
S.L.P 2888,
40470DODOMA

## TAARIFA KWA UMMA

1. Ndugu mwananchi mnatangaiwa tarehe 13/11/2020 kampuni ya **chico (china henan internation cooperation group co.ltd)** itasafirisha mzigo (32 counter attack liner) wake wenye vipimo vikubwa kutoka **DODOMA** kuelekea **TABORA kupitia ITIGI,** gari hilo lenye namba za usajiri **T507 BKM / T509 BKM,** yenye escort no **T643 CVZ**
2. Gari hilo linavipimo vifuatavyo
   **Urefu - mita 20.00m**
   **Upana - mita 3.00m**
   **Kimo - mita 4.5m**
3. Njia itakayo tumika ni **DODOMA hadi TABORA kupitia ITIGI**
   Gari itasafiri muda wa mchana tu kuanzia saa 12:30 asubuhi mpaka saa 12:00 jion

*Tunaomba radhi kwa usumbufu*

**JAMHURI YA MUUNGANGO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455.
Fax: +255 26 2323233.
Barua Pepe: ps@mow.go.TZ.
Tovuti: www.mwtc.go.TZ.

Mtaa wa Moshi
S.L.P 2888,
40470DODOMA

## TAARIFA KWA UMMA

1. Ndugu mwananchi mnatangaiwa tarehe 17/11/2020 kampuni ya chico **(china henan internation cooperation group co.ltd)** itasafirisha mzigo **(Machine TAMPING ROLLER)** wake wenye vipimo vikubwa kutoka **TABORA kuelekea DODOMA kupitia ITIGI ,** gari hilo lenye namba za usajiri **T507 BKM / T509 BKM,** yenye escort no **T643 CVZ**
2. Gari hilo linavipimo vifuatavyo
   **Urefu - mita 20.00m**
   **Upana - mita 3.00m**
   **Kimo - mita 4.5m**
3. Njia itakayo tumika ni **TABORA hadi DODOMA kupitia ITIGI**
   Gari itasafiri muda wa mchana tu kuanzia saa 12:30 asubuhi mpaka saa 12:00 jion

*Tunaomba radhi kwa usumbufu*

**Uza,**
**Chenye Thamani**
**Kubwa Kwa Kutangaza**
**Nasi Kwa Bei Poa**
**Tupigie 0782253676**

**MAHAKAMA YA ARDHI NA NYUMBA YA WILAYA MBEYA**
**SHAURI NO.180/2015**
**AMBELE MASUBA..............................MDAI**
**Versus**
**MATRIDA SIMON MWAKYONYA.............................. MDAIWA**
**VITUS MHAGAMA..............................MDAIWA**
**MBEYA CITY COUNCIL..............................MDAIWA**
**RAFAEL MWAIKONO..............................MDAIWA**
**YAH : KUITWA SHAURINI**

**KWA :**
**VITUS MHAGAMA**
Fahamu kwamba **AMBELE MASUBA** amefungua shauri dhidi yako katika baraza hili.
Shauri limepangwa kutajwa tarehe 19/11/2020 saa 3:00 asubuhi mbele ya Mh.A.Mapunda Mwenyekiti wa Baraza.
Unatakiwa kuleta utetezi wa maandishi ndani ya siku 21 tangu tarehe ya wito huu.
Nyaraka zinazohusu shauri hili zinapatikana katika masijala ya Baraza la Ardhi na Nyumba Mbeya.
Unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa wewe mwenyewe au mwakilishi anayeruhusiwa kisheria.Ofisi za baraza zipo ndani ya eneo la Sabasaba Mbeya mjini.
**Kumbuka:** Usipo hudhuria siku hiyo baraza litatoa amri stahilivu ikiwa ni pamoja na kusikiliza shauri pasipo wewe kuwepo.
Amri hii imetolewa kwa mkono wangu na Lakiri/Muhuri wa baraza hili leo tarehe 04/11/2020.

**A.Mapunda**
**MWENYEKITI**
**04/11/2020.**

**Kwa Habari Motomoto**
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676
Nipashe
MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HADITHI

# Mauaji Harusini-38

ILISEMWA hapo zamani kuwa dunia inaharibiwa na vitu viwili tu. Mapenzi na mali. Vitu hivi vinaweza kumfanya binadamu aende popote. Afanye chochote kile ili awe navyo, wengine wanakwenda mbali zaidi mpaka ikiwezekana hata kutoa uhai wa wenzao.
Shani, binti wa kitajiri anapitia kwenye mikasa mikubwa mizito ya kupotezwa kwa wazazi wake na kumsababishia ukiwa na mawazo tele.
Wakati ikionekana binti huyo pekee kwa wazazi wake akielekea kurithi utajiri wa wazazi wake, kiu ya damu inaanza kuwaingia baadhi ya ndugu za wazazi wake ili apoteze maisha, wao waweze kumiliki mali hizo.
Hapo ndipo uhai wa Shani unapokuwa matatani na patashika nguo kuchanika inapoanza. Fuatilia mkasa huu kuburudisha, kuelimisha na kusikitisha.

**Na Adam Fungamwango, (0716 350534)**

ILISEMWA hapo zamani kuwa dunia inaharibiwa na vitu viwili tu. Mapenzi na mali. Vitu hivi vinaweza kumfanya binadamu aende popote. Afanye chochote kile ili awe navyo, wengine wanakwenda mbali zaidi mpaka ikiwezekana hata kutoa uhai wa wenzao.

Shani, binti wa kitajiri anapitia kwenye mikasa mikubwa mizito ya kupotezwa kwa wazazi wake na kumsababishia ukiwa na mawazo tele.

Wakati ikionekana binti huyo pekee kwa wazazi wake akielekea kurithi utajiri wa wazazi wake, kiu ya damu inaanza kuwaingia baadhi ya ndugu za wazazi wake ili apoteze maisha, wao waweze kumiliki mali hizo.

Hapo ndipo uhai wa Shani unapokuwa matatani na patashika nguo kuchanika inapoanza. Fuatilia mkasa huu wa kuburudisha, kuelimisha na kusikitisha.

==================================================

"Mpenzi, nimepata taarifa kuwa baba zangu wadogo George na Paul wamekamatwa." Sauti ya Shani ilipenya kwenye masikio ya Eddy. Ilikuwa ni muda mfupi tu baada ya kuwasili nyumbani kwao Kijitonyama.

Shani na Eddy sasa waliishi pamoja. Ni baada ya tukio la Mbezi Beach ambalo watu wawili walivamia kwenye nyumba ya Shani kwa nia ya kutaka kumdhuru kwa kutumwa na Jim na ndugu zake.

"We nani kakupa hiyo taarifa?" Eddy aliuliza kwa mshangao.

"Mama mdogo Marina, mke wa George kaniambia kuwa mumewe ana wiki sasa amekatwa, na tayari baba mdogo Ben amekamatwa na yeye."

"Mmmh, kwani wamefanya nini hadi wakamatwe mtu na ndugu yake?" Eddy alihoji kinafiki kwani alifahamu kila kitu na yeye ndiye mhusika mkuu wa kuwatia wote hao mbaroni.

"Mwenzangu, hata sielewi, halafu nimeambiwa kuwa baba mkubwa Jim na Ben hawaonekani nyumbani, sijui imekuwaje?" Shani alilalama kwa namna ya masikitiko.

"Labda na wao watakuwa wamekatwa ila vituo tofauti, inabidi na wao watafutwe kwenye vituo vingine."

"Inawezekana eee, kweli wewe umesema, ngoja nimpigie mama mdogo nimwambie?"




Eddy alimtazama Shani jinsi alivyokuwa amehamanika kutokana na baba zake wadogo na wakubwa kukamatwa.

"Laiti angejua kuwa mimi ndiye niliyetoa amri ya kuwatia mbaroni? Laiti angekua kuwa kosa lao ni kutaka kumuua yeye ili wachukua utajiri wa baba yake..." Eddy alijisemea moyoni huku akimtazama kwa makini Shani.

"Mbona kama unanishangaa sana Eddy?" Aliuliza.

"Umependeza."

"Yaani huko kote hukuniambia, uje kuniambia huku."

"Sikutaka watu wasikie ninavyokusifia."

Siku zote Shani anafahamu kuwa Eddy ni mtu wa mzaha. Akamuacha kama alivyo, huku akitabasamu.

Kama kawaida Eddy aliifanya kazi yake kwa ustadi mkubwa. Mpaka sasa, pamoja na kuwa wote kama wapenzi, lakini Shani alikuwa hajagundua kuwa anaishi na mpelelezi mashuhuri nchini Tanzania, Eddy Kamal.

Hajagundua kama alikuwa amewekewa sumu kwenye chakula siku ile kule ABC Hotel ili afe taratibu.

Alikuwa hajui chochote kuwa Eddy alimponya kwenye mkasa huo, kiasi cha kusababisha baadaye kifo cha Fikiri aliyepewa kazi ya kuweka sumu.

Alikuwa hajui kuwa waliovamia nyumbani kwake walikuwa na lengo lile lile la kutaka kummaliza. Alieyelewa hilo ni Eddy pekee. Yeye alidhani ni wezi tu.

Sababu kubwa ya Eddy kufanya hivyo ni kutomtisha. Alitaka msichana huyo aishi kwa amani. Angejua kuwa kuna watu wanamfuatilia wamuue, asikuwa na amani na furara tena. Angejua ndugu zake ndiyo wanataka kumuua, angeshangaa na kukosa raha. Kila ktu alipanga kumaliza yeye kabla ya Shani kudhurika. Ndiyo maana leo amemtoa Mbezi Beach na kumleta kwake Kijitonyama.

**************************

Haikuwa ghafla kama Shani alivyodhani. Eddy alishaliona lile dakika 20 zilizopita. Wakati akitoka maeneo ya Posta mpya kumchukua Shani, kupitia barabara ya Bagamoyo alihisi kuna gari ilikuwa inawafuatilia.

Halikuwa gari tu, bali kulikuwa pia na bodaboda ambayo ilionekana kama ina safari zake, lakini ilikuwa haiwapiti.

Ajabu sana bodaboda kukaa nyuma ya gari kwa muda mrefu. Maajabu ya bodaboda kushindwa kuzipita gari, ndiyo yaliyomfanya Eddy kuwa makini. Umakini huo ulimfanya kugundua kuwa kuna gari lingine aina ya Subaru Forester rangi ya bluu. Ilionekana kuwa karibu mno na bodaboda hiyo aliyoitilia mashaka.

Kulikuwa kama kuna mawasiliano kati ya watu wawili waliokuwa wamepanda boda hiyo na waliokuwa ndani ya gari hilo.

Akiwa ndani ya Mercedes Benz E200, ikiwa ni moja kati ya gari zilizonunuliwa hivi karibuni na Shani kutokana na mapendekezo yake ya kutotumia aina moja ya gari kwa muda mrefu kwa ajili ya usalama, Eddy alijua hakukuwa na usalama hata chembe.

Damu ilimsisimka. Kwa muda mrefu hajawahi kukutana na kitu kama hicho. Kwa muda mrefu amekuwa huru, japo kulikuwa na matukio ya hapa na pale.

Alichohofia zaidi ni mtu aliye ndani ya gari. Angekuwa peke yake, wala asingewaza sana. Alijua kabisa kuwa kitakachotokea, ndiyo kitakuwa mwanzo wa Shani kujua kila kitu. Lakini pia kujua siku zote alikuwa akimficha mambo mengi. Hata hivyo aliwaza kuwa lolote litakalotokea, atamwambia alifanya hivyo kwa sababu anampenda. Hakutaka akae na mawazo au kwa hali ya wasiwasi, ila mwisho wa siku alijua kuwa atagundua, lakini hatari itakapokuwa imekwisha.

Hata hapo hakutaka kumshtua kabisa Shani kama kuna watu wanawafuata.

Kwa akili ya haraka haraka ya kiitelejensia, Eddy alianza kuendesha gari kwa haraka, licha ya foleni za hapa na pale kwenye jiji la Dar es Salaam.

Alipolipita daraja la Salenda mbele, alitaka barabara inayoelekea Kinondoni, badala ya kwenda moja kwa moja hadi maeneo ya Morocco.

Haikuwa na magari mengi upande ambao watu wanatoka mjini kurudi majumbani. Sasa alijua kwa asilimia 100 kuwa walikuwa wanafuatwa. Bodaboda nayo ilikata kona na kuzidisha mwendo kwa kasi. Gari lile nalo likuwa nyuma nalo likakata kona ile ile. "Hii siyo bahati mbaya." Aliwaza.

Saa ndogo iliyokuwa ndani ya gari lao ilionyesha kuwa ni 12:30 jioni. Kwa hali ya hewa ya Dar es Salaam ambayo mchana kulikuwa na mvua, jua lilipoteza nuru yake na giza likaanza kutawala kwa nguvu, licha ya mwanga wa taa za barabarani zilizokuwa zikijaribu kupigana na nguvu za giza ambalo lilioonekana kuwa shujaa, mara baada ya jua kusalimu amri.

"Lala chini Shani." Amri ilitoka kwa Eddy, ikifuatiwa na vitendo, mkono mmoja ukimvua mkanda na kumshika kichwa kukipeleka chini.

Kilikuwa ni kitendo ambacho Shani hakukitegemea, kwani muda wote alikuwa akichezacheza kwenye gari, akideka na kula bisi, pamoja na kunywa juisi.

Ile kasi ya gari ilivyokuwa ikiendeshwa kwa namba ambayo hajawahi kuiona, tena ikiendeshwa na mpenzi wake, ilimtisha kuliko kutisha kwenyewe.

Alianza kupunguza kasi ya gari ili bodaboda ikaribie. Alishajua nini walihitaji. Wakati ikifika karibu na dirisha, ghafla alifunga breki.

Waliokuwa kwenda bodaboda hawakutegemea hilo, hivyo alipitiliza. Hapo hapo milio kadhaa ya risasi ilimiminika.

Ilipopigwa ni eneo ambalo lilitakiwa gari la Eddy na mpenzi wake Shani liwe. Kitendo bila kuchelewa, Eddy alimbeba Shani kama simba ananyombeba nyati. alibimbirika naye kwenye viti vya nyuma. Alijua kabisa kuwa watu hao walidhamiria kuwateketeza kwa risasi. Hivyo alijua risasi zitakazofuata baada ya kuwakosa, zitamiminika eneo la mbele la gari lao. Na ndivyo ilivyokuwa. Wakati gari la lilikuwa likifuata nyuma likimimina risasi zake kupitia kioo cha nyuma na kwenda kuvunja kioo cha mbele. Bodaboda iliyokuwa imepitiliza mbele nayo iligeuka nyuma na kuifuata gari waliyokuwepo kina Eddy. Nao wakamimina risasi za kutosha na kuichakaza gari hiyo kwa tundu.

***Itaendelea Jumamosi***

# SCALONI ALIA MESSI KUNYIMWA BAO



**BUENOS AIRES,** Argentina

LIONEL Scaloni ametaka matumizi ya VAR kuangaliwa kwa umakini zaidi baada ya Argentina kunyimwa ushindi dhidi ya Paraguay.

Nicolas Gonzalez alisawazisha bao la penalti la Angel Romero pale La Bombonera Alhamisi na Argentina walionekana kama wangeondoka na ushindi wa tatu mfululizo wa kufuzu michuano ya Kombe la Dunia, wakati Lionel Messi alipofunga goli la pili.

Hata hivyo, bao hilo lilikataliwa baada ya uhakiki wa VAR, kwamba kulikuwa na faulo na hivyo vijana hao wa Scaloni wakafikisha pointi saba katika mechi tatu za kufuzu Kombe la Dunia mwaka 2022.

Lakini kocha huyo wa Argentina anataka VAR kuwa na matokeo halisi, kwani walinyimwa ushindi wao.

"Nafikiri ni muhimu kuwa na umoja kwenye ili suala la VAR," alisema Scaloni akiwaambia waandishi wa habari.

# Liverpool yafikia pazuri kwa Skriniar

**LIVERPOOL,** England

KLABU ya Liverpool imeanzisha mipango ya kutaka kumsajili mlinzi wa kati wa Inter Milan, Milan Skriniar, kwa mujibu wa ESPN.

Jurgen Klopp anafahamu wazi anahitaji beki wa kati baada ya Virgil van Dijk kuumia na kwamba atakuwa nje ya uwanja karibu msimu mzima.

Kwa sasa, Klopp anawategemea Joe Gomez, Fabinho, Nat Phillips na Rhys Williams kwenye kuimarisha safu yake ya ulinzi, huku Joel Matip akirudi kutoka majeruhi na alikuwapo uwanjani Jumapili kwenye mchezo dhidi ya Manchester City.

Kwa mujibu wa ripoti, miamba hao wa Anfield wapo kwenye mpango wa kumsajili Skriniar ambaye kwa muda mrefu amekuwa kwenye rada za Jose Mourinho.

Ripoti zinadai kwamba Liverpool imepiga hatua nzuri katika mazungumzo na Inter Milan kwa ajili ya beki huyo ambaye anaweza kupatikana kwa euro milioni 60.

Skriniar uchezaji wake anafananishwa na Martin Skrtel, beki wa zamani wa Liverpool, lakini kama Klopp atafanikiwa kunasa saini yake basi jambo hilo hilo bila shaka litamtibua sana Mourinho.

Kutokana na hilo pengine kunaweza kutokea vita kali baina ya makocha hao wawili, Klopp na Mourinho katika kunasa huduma ya beki huyo wa kimataifa wa Slovakia





# *Southgate asifia England ya vijana*

**LONDON,** England

GARETH Southgate amekisifia kikosi cha England kilichokuwa na wachezaji wasio wazoefu katika ushindi wa 3-0 dhidi ya Jamhuri ya Ireland kwenye mchezo wa kirafiki.

Kikosi hicho kilikuwa bila wachezaji wengi wazoefu kama Jordan Henderson, Raheem Sterling na Harry Kane kwenye mchezo huo uliopigwa pale katika dimba la Wembley, juzi Alhamisi.

Badala yake Southgate aliamua kuwatumia vijana, huku golikipa Nick Pope mwenye umri wa miaka 28 ndio alikuwa mchezaji mwenye umri mkubwa zaidi kwenye kikosi hicho.

Huku Jude Bellingham aliingia kwenye rekodi ya kuwa mchezaji mwenye umri mdogo zaidi kuichezea England- akishika nafasi ya tatu nyuma ya Theo Walcott na Wayne Rooney.

"Kwa uhakika kabisa nilifurahishwa mno na wachezaji hawa vijana," alisema Southgate akiiambia ITV

"Kuwa na kundi la wachezaji vijana kama hawa ambao hawana uzoefu na kupata matokeo mazuri, hakika ni jambo bora zaidi kwetu.

"Kubwa zaidi ni kwamba, tulipata ushindi na kundi la wachezaji vijana, ambao hawana uzoefu."

HABARI MICHEZO

# Makamu wa Rais wa FIFA ajiuzulu

**NYON,** Uswisi

SHIRIKISHO la Umoja wa Vyama vya Soka Ulaya, UEFA, imethibitisha kuwa Greg Clarke amejiuzulu nafasi ya Makamu wa Rais wa Shirikisho la Soka la Kimataifa (FIFA).

Bosi huyo mwenye umri wa miaka 63, alijiuzulu nafasi hiyo kutokana na maoni ya kukera juu ya vikundi vya watu wachache.

Lakini, baada ya kuchaguliwa na UEFA mwaka jana, hapo awali alikuwa amepanga kubaki katika wadhifa wake wenye mshahara wa pauni 190,000 kwa mwaka, ambao unaendelea hadi 2023.

Msemaji wa UEFA alisema: "Kufuatia mazungumzo ya njia ya simu kati ya Rais wa UEFA na Greg Clarke, walikubaliana na pendekezo lake kwamba, aondoke madarakani mara moja kutoka katika nafasi yake ya mwakilishi wa UEFA kwenye Baraza la FIFA."

Clarke hapo awali alisisitiza kwamba alibaki madarakani kwa sababu tu ya ombi kutoka kwa rais wa UEFA, Aleksander Ceferin kwamba afanye hivyo.

"Ninakaa kwa ombi la rais wa UEFA Aleksander Ceferin," alisema.

Uamuzi huo tayari ulikuwa umesababisha hasira ndani ya jamii ya mpira wa miguu,

FIFA inazingatia kwamba Clarke alifanya jambo sahihi kujiuzulu wadhifa wake huo.

Clarke alichaguliwa katika nafasi yake kwenye Baraza la FIFA na UEFA na muda wake wa kazi unaendelea hadi 2023.






# INTER YAMJIBU KOCHA WA CHILE JUU YA SANCHEZ

**MILAN,** Italia

INTER Milan imetoa taarifa za kujibu tuhuma za Kocha Mkuu wa Chile, Reinaldo Rueda, ambaye alidai Nerazzurri hao walimtumia sana Alexis Sanchez.

Klabu hiyo ya Serie A, iliingia kwenye mgogoro na Chile juu ya Sanchez, huku klabu hiyo ikitaka wachezaji wasihusishwe kwenye mechi za kimataifa kwa sababu ya mlipuko wa virusi vya corona.

Rueda aliishutumu Nerazzurri kwa kutoonyesha heshima, lakini miamba hao wa Serie A, wamejibu, wakisema kwamba kauli hiyo ya kocha haikubaliki.

Taarifa ya Klabu ilisema: "Klabu mara zote imekuwa na mahusiano mazuri na benchi la ufundi la timu za taifa.

"Katika suala la Alexis Sanchez, mchezaji mwenyewe amekuwa na matatizo ya kiafya kabla ya kuitwa timu ya taifa. "Mojawapo ni kwamba aliumia na kulazimika kukaa nje ya dimba kwa zaidi ya mezi mitatu.

"Hivyo kauli ya kocha wa Chile haikubaliki na hakupaswa kuitoa kwa kuilaumu Inter Milan."

# *Majeruhi yazidi kuitesa Liverpool*

**LIVERPOOL,** England

KLABU ya Liverpool imethibitisha mlinzi wake wa kulia, Trent Alexander-Arnold atakuwa nje ya uwanja wa karibia wiki nne.

Trent aliumia katika mchezo uliopita wa Ligi Kuu England, dhidi ya Manchester City ambao ulimalizika kwa sare ya bao 1-1.

Majeraha hayo yamemfanya kuongeza idadi ya wachezaji wa timu hiyo ambao wapo nje ya dimba kutokana na majeruhi waliyopata kuanzia mwanzo wa msimu.

Kocha wa wekundu hao wa Anfield, Jurgen Klopp alithibitisha kwamba majeraha aliyoyapata mchezaji huyo sio madogo na yatamweka nje ya uwanja wa zaidi ya wiki tatu.

Akitegemea kumkosa kwenye michezo kadhaa ijayo ikiwa ile ya Leicester, Brighton na Wolves, na michuano ya Ligi ya Mabingwa dhidi ya Atalanta na Ajax, ambazo zote zitapigwa pale Anfield.

Mbali ya Trent ambaye ameondolewa kwenye kikosi cha timu ya Taifa ya England, Liverpool inaendelea kumkosa Virgil van Dijk, Thiago Alcantara na Alex Oxlade-Chamberlain.



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# WOODWARD: TUNA IMANI NA SOLSKJAER

Bosi huyo wa United aweka wazi huku akisema kocha huyo bado anaendelea...

**MANCHESTER,** England

MANCHESTER United "ina imani kubwa" na Ole Gunnar Solskjaer kama kocha wa klabu hiyo, amesema Makamu Mwenyekiti Mtendaji, Ed Woodward.

**Majaliwa ya Solskjaer yalizua maswali baada ya kupokea vichapo mfululizo hivi karibuni kutoka kwa Arsenal na Istanbul Basaksehir.**

Hata hivyo, ushindi wa wiki iliyopita wa mabao 3-1 dhidi ya Everton uliinyanyua United hadi nafasi ya 14 kwenye msimamo wa Ligi Kuu England na kupunguza presha kwa raia huyo wa Norway.

Na wakati akitambua kuna ishara ya maendeleo, Woodward amemtetea Solskjaer kuendelea kuinoa United.

"Kwenye dimba, huku kukiwa na kazi ngumu ya kuimarisha mafanikio ya mwendelezo wa ushindi, tunabakia kuwa na imani kubwa na mtazamo chanya kwa Ole kuendelea kuiendeleza timu," alisema bosi huyo.

Kauli ya Woodward imetolewa sambamba na matokeo ya mapato ya kifedha kwa robo ya mwaka, ambayo ilitolewa mapema kimakosa.

Mapato ya United yameshuka kwa asilimia 20 kwa miezi mitatu kufikia Septemba 30, mwaka huu, kutoka pauni milioni 135.4 hadi pauni milioni 109 ikilinganishwa na wakati kama huo mwaka jana.

Na kushuka kwa mapato hayo ni kutokana na mashabiki kutoruhusiwa kuingia uwanjani, lakini Woodward ana matumaini mashabiki hivi karibuni wataruhusiwa na kurudi katika dimba la Old Trafford.

"Tumewamisi mashabiki wetu, kucheza bila mashabiki kunafanya wachezaji wasiwe na molari kubwa.

"Lakini naamini mambo haya yatamalizika hivi karibuni na mashabiki wataruhusiwa kuingia viwanjani."

## ZISIKUPITE

### RONALDO KUREJEA UNITED

MANCHESTER United wamewasilisha rasmi dau la kumnunua, Cristiano Ronaldo (35), kwa wakala wake, katika jaribio la kumsajili nyota huyo wa Ureno kutoka Juventus. Mabingwa hao wa Serie A wako tayari kumwachilia straika endapo wasiposhinda Ligi ya Mabingwa Ulaya. ***(Record, via Sport Witness)***

### BOATENG AGOMBEWA EPL

ARSENAL, Chelsea na Tottenham zinamtaka beki wa Bayern Munich, Jerome Boateng. Mjerumani huyo mwenye umri wa miaka 32, huenda akaondoka huru baada ya kukamilisha mkataba wake mwishoni mwa msimu huu. ***(Bild, Sun)***

### TRAORE AIVURUGA WOLVES

KLABU ya Wolves imeaanza kukwazika na winga wao, Adama Traore ambaye hajatia saini mkataba mpya. Kiungo huyo wa kimataifa wa Hispania, mwenye umri wa miaka 24 wiki iliyopita alikubali mkataba mpya kwa masharti, lakini hajajitokeza kuutekeleza. ***(90min)***

### CHELSEA YAMGANDA RICE

CHELSEA inatarajia kuwasilisha dau lingine la kumnunua kiungo wa kati wa West Ham na England, Declan Rice wakati wa dirisha la Januari. The Blues hao watawauza wachezaji wawili wakubwa ili kufadhili uhamisho wa Rise mweye umri wa miaka 28. ***(Football Insider)***

### LIVER KUMNASA JANMAAT

LIVERPOOL wanatafakari uwezekano wa kumnunua mlinzi wa zamani wa Uholanzi na Watford, Daryl Janmaat, ambaye ana umri wa miaka 31, kama hatua ya muda mfupi ya kuimarisha safu yake ya ulinzi inayokabiliwa na changamoto. ***(Teamtalk)***

### UPAMECANO SOKONI

KLABU ya Liverpool pia inamwania mlinzi wa RB Leipzig na Timu ya Taifa ya Ufaransa, Dayot Upamecano, ambaye ana umri wa miaka 22 na yuko kwenye orodha ya kuimarisha zaidi safu yao ya ulinzi. (The Athletic)

### AKARIBIA ARSENAL

ARSENAL wamepata matumaini mapya katika jaribio lao la kumsajili kiungo wa kati wa RB Salzburg, Dominik Szoboszlai mwenye umri wa miaka 20, baada ya wakala wa mchezaji huyo raia wa Hungary kukanusha madai kwamba anahamia RB Leipzig. ***(Mirror)***

### BILIC MAMBO MAGUMU

HATIMA ya Kocha wa West Brom, Slaven Bilic haijulikani huku klabu hiyo ikiendelea kuwa na matokeo mabaya kwenye Ligi Kuu England msimu huu, tetesi zinaarifu Lee Bowyer wa Charlton ni miongoni mwa majina yanayopigiwa upatu kuchukua nafasi yake. ***(Mirror)***

### ERIKSEN AJUTIA UAMUZI

KIUNGO wa kati wa zamani wa Denmark na Tottenham, Christian Eriksen mwenye umri wa miaka 28, anasema hali yake ya sasa "haikua ndoto yake". ***(TV2, via Goal)***

### NYOTA MADRID KUBANWA

KLABU ya Real Madrid inatarajiwa kuwapunguzia tena marupurupu wachezaji wake kutokana na athari za janga la virus vya corona. ***(ESPN)***

## Ligi ya Muungano netiboli yakaribia

**Na Shufaa Lyimo**

CHAMA cha Netiboli Tanzania (CHANETA), kimezikumbusha timu zote zinazoshiriki Ligi ya Muungano itakayofanyika kuanzia Novemba 28, mwaka huu jijini Tanga, kufika mapema kwenye kituo cha mashindano hayo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu Mkuu wa Chaneta, Judith Ilunda, alisema wanahitaji kuona timu zinawahi kituoni ili kuepusha usumbufu na kukamilisha maandalizi.

"Tunaomba timu zote ambazo zitashiriki mashindano hayo zifike mapema Tanga, hii itatufanya tujiepushe na usumbufu," alisema Ilunda.

Kiongozi huyo alisema maandalizi ya ligi hiyo itakayoshirikisha timu za Tanzania Bara na Visiwani Zanzibar yako katika hatua za mwisho na wanategemea kuona ushindani zaidi mwaka huu.

"Tumeona maandalizi ya baadhi ya timu, yametuvutia, tunatarajia kuona mvuto kwa sababu ya maandalizi yaliyofanywa na pande zote," Ilunda alisema.

Aliwataka Watanzania kujitokeza kushuhudia mashindano hayo yatakapoanza kwa ajili ya kuona vipaji katika mchezo huo.

## BMT yakumbusha vyama kusajiliwa

**Na Jumbe Ismailly,** SINGIDA

BARAZA la Michezo la Taifa (BMT), limevitaka vyama vyote vya michezo mkoani hapa kuhakikisha vinakamilisha usajili wa kudumu kama kanuni zinavyoelekeza, imeelezwa.

Agizo hilo limetolewa na Ofisa Maendeleo ya Michezo wa Manispaa ya Singida, Samuel Mwaikenda wakati wa kufunga Mkutano Mkuu wa uchaguzi wa Chama cha Riadha Singida uliofanyika juzi.

Mwaikenda ambaye pia ni Msajili Msaidizi wa vyama pamoja na vilabu alisisitiza Chama ambacho hakitakuwa na usajili, hakitaruhusiwa kufanya kazi zake na hakitatambulika kisheria.

"Vyama vya michezo vinatakiwa visajiliwe, sio ombi ni sheria, ni lazima visajiliwe kwa sababu vikisajiliwa ndio vinakuwa vinatambulika na suala hili sisi kama maofisa michezo tumejipanga kuanza nalo kwa umakini," alisisitiza Mwaikenda.

Kiongozi huyo alisema zoezi la kuhakiki vyama vilivyosajiliwa kuanzia ngazi ya wilaya linatarajiwa kufanyika hivi karibuni na kuhimiza wasimamizi kukamilisha mchakato huo bila ya mizengwe.

"Nashukuru hadi sasa vyama vingi vimeshaanza mchakato na wengine wameshakamilisha kuandaa katiba, na wengine katiba zao zimeshaenda kwa msajili," Mwaikenda aliongeza.

Alisema pia BMT imejipanga kutoa elimu kwa viongozi wa vyama hivyo ili kumaliza sintofahamu ya katiba zao na hivyo wanakwamba kukamilisha mchakato wa usajili.

# SIMBA SC YAMWINDA NAHODHA WA BIASHARA

**Na Adam Fungamwangwo**

WAKATI kipindi cha dirisha dogo la usajili kikikaribia, mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba, wanatajwa wako kwenye mipango ya kuwania huduma ya beki wa kati na nahodha wa Biashara United, Abdulmajid Mangalo.

**Lengo la kumsajili beki huyo ni kutaka kuongeza nguvu kwenye safu ya ulinzi ili kufanya vyema katika Ligi Kuu Tanzania Bara na mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.**

Mwenyekiti wa Klabu ya Biashara United, Selemani Mataso alisema ingawa bado Simba haijakwenda rasmi kufanya mazungumzo nao, lakini tayari kuna tetesi zimeanza kusikika kuhusiana na beki huyo kutakiwa na mabingwa hao watetezi.

"Nimesikia, lakini hawajaja kwetu rasmi. Ila wakija sisi tuko tayari kumwachia wala hatuna tatizo. Hatuwezi kukaa na mchezaji wakati anatafuta maisha, ila tu ninachowataka wasitumie mbinu za 'panya', bali waje kwetu, wala hatutokuwa na matatizo nao kama wakifuata taratibu," alisema Mataso.

Mwenyekiti huyo alisema mara nyingi kipindi cha usajili kila klabu inawinda wachezaji wazuri, hivyo hata wao watauza wachezaji na kusajili wengine kulingana na mahitaji ya timu.

Alisema beki huyo bado ni mali ya Biashara kwa sababu amebakiza mkataba wa mwaka mmoja wa klabu hiyo.

"Hiki ni kipindi cha dirisha dogo, mchezaji mzuri ndiye atakayechukuliwa na mchezaji wetu ni mmoja kati ya wachezaji wazuri, kila timu inamtaka, wala si tatizo, tutakaa kwenye mazungumzo kila kitu kitaenda sawa," alisema Mataso.

Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Haji Manara, hajasema lolote kusiana na mchezaji huyo, lakini amekiri klabu hiyo haiwezi kumkosa mchezaji yoyote itakayomhitaji, si Tanzania tu, bali ukanda wote wa Afrika Mashariki na Kati.

Simba inaonekana kutaka kurekebisha safu yake ya ulinzi baada ya kuonekana ina upungufu katika mechi zake 10 ilizocheza za Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu.



Mshambuliaji wa Timu ya Soka ya vijana ya umri chini ya miaka 20 (Ngorongoro Heroes), Anuary Bakary (katikati), akijaribu kumiliki mpira dhidi ya nyota kutoka Sudan katika mechi ya kirafiki ya kimataifa iliyochezwa kwenye Uwanja wa Uhuru jijini, Dar es Salaam hivi karibuni. Ngorongoro Heroes ilifungwa mabao 2-1. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Ngorongoro, Lyon hakuna mbabe

**Na Saada Akida**

KIKOSI cha Timu ya Soka ya Taifa ya vijana ya umri chini ya miaka 20 ( Ngorongoro Heroes) na African Lyon zimeshindwa kutambiana baada ya kutoka sare ya mabao 3-3 katika mchezo wa kirafiki uliopigwa kwenye Uwanja wa Uhuru jijini, Dar es Salaam jana asubuhi.

Mabao ya Ngorongoro Heroes yalifungwa na Neno Modest aliyefunga magoli mawili pamoja na Ashraf Maloto wakati kwa upande wa African Lyon inayoshiriki Ligi Daraja la Kwanza yalipachikwa wavuni na Mussa Gadi, Mwalami Abdallah na Abu Malik.

Ngorongoro Heoers inayojiandaa na mashindano ya Afrika Mashariki na Kati (Cecafa U-20), kitashuka tena dimbani leo kucheza mechi nyingine ya kirafiki dhidi Namungo FC kwenye Uwanja wa Uhuru.

Kocha Mkuu wa timu hiyo, Jamhuri Kihwelo 'Julio' alisema mechi hizo ni kwa ajili ya kuendelea kukiimarisha kikosi chake na kuwapa nafasi wachezaji kuzoeana.

"Hii ni mechi ya pili kutoka sare kati ya michezo mitatu ya kirafiki tuliyocheza, imenipa mwanga na kuona upungufu wa kikosi changu lakini pia kuanza kupata kikosi cha kwanza kwa ajili ya maandalizi ya michuano ya Cecafa," alisema Julio.

Ngorongoro Heroes ndio mwenyeji wa michuano ya CECAFA U-20 mwaka huu ambayo inatarajia kufanyika kuanzia Novemba 20 hadi Desemba 6, mwaka huu jijini, Arusha na Karatu.

# Michezo

Jumamosi Novemba 14, 2020

Nipashe



Woodward: Tuna imani na Solskjaer UKURASA 22



Kiungo wa Timu ya Taifa ya England, Dominic Calvert-Lewin (kushoto), akifunga bao la tatu kwa timu yake katika mechi ya kirafiki ya kimataifa dhidi ya Ireland, iliyochezwa kwenye Uwanja wa Wembley jijini London, juzi usiku. England ilishinda mabao 3-0. **PICHA: MTANDAO**

## Magufuli atangaza neema michezoni

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

RAIS Dk. John Magufuli (pichani) amesema Watanzania wanataka ushindi kwenye michezo kwa sababu wamechoka kushindwa.

Akizungumza bungeni jijini hapa jana, wakati akizindua bunge la 12, Rais Magufuli alisema "Watanzania tunakata ushindi, tumechoka 'kushindwa shindwa'."

Magufuli alisema pia kwa miaka mitano ijayo, Serikali itatenga fedha kidogo kidogo kwa ajili ya kuziandaa timu za taifa zinazokwenda kushiriki katika mashindano mbalimbali ya kimataifa.

Aidha, alisema Serikali itaendelea kuimarisha sekta ya Sanaa, Utamaduni na Michezo ambazo zinakua kwa kasi hivi sasa hivi.

"Ninaahidi kuhuisha Mfuko wa Sanaa na Utamaduni ili kuwasaidia wasanii kupata mafunzo ya sanaa pamoja na mikopo," alisema Magufuli.



Alisema Serikali itaimarisha usimamizi wa haki miliki za wasanii ili wanufaike na kazi zao pamoja na kuchangia pato la taifa.

# Simba, Yanga hadithi ile ile

**Na Adam Fungamwango**

## ●●● Msimbazi 'yachafua' hali ya hewa baada ya kutajwa inamwania Tonombe katika dirisha dogo...

KLABU ya Simba imesema inatarajia kufanya usajili wa 'kishindo' ambao utashtua mashabiki na wadau wa soka nchini na Afrika Mashariki na Kati katika kipindi cha dirisha dogo ili kuimarisha kikosi kinachoratajiwa kushiriki mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

**Simba ndio mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara na wamejipanga kutetea taji hilo wanalolishikilia kwa mwaka wa tatu mfululizo pamoja na kufanya vyema kwenye michuano ya kimataifa watakayoshiriki.**

Wekundu hao wa Msimbazi pia ndio mabingwa wa michuano ya Kombe la FA, ambapo fainali walicheza na Namungo FC ya Lindi.

Taarifa ambazo zimeendelea kutawala zinadai Simba imeanza mazungumzo na kiungo mkabaji wa Yanga ambaye ni raia wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Mukoko Tonombe.

Tetesi hizo zilianza kusambaa baada ya watani zao kuonyesha pia wanamipango ya kumsajili kiungo wa Simba Mzambia, Clatous Chama.

Akizungumza na gazeti hili jijini, Dar es Salaam jana, Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Haji Manara alisema lengo la kufanya usajili wa kiwango bora ni kuboresha kikosi chao ambacho kimeweka malengo ya kufanya vyema kwenye michuano ya kimataifa msimu huu.

Manara alisema klabu yao ina uwezo wa kumsajili mchezaji yoyote yule kwenye ukanda wa Afrika Mashariki na Kati, kwa sababu wachezaji wengi wanapenda kuichezea klabu hiyo kutokana na historia yake.

"Mchezaji mzuri yoyote anataka kucheza mechi za kimataifa, haiwezekani mchezaji mzuri akakaa tu kucheza mechi za kawaida tu humu ndani, tumejipanga kusajili yoyote ambaye mwalimu atamhitaji," alisema na kuongeza.

"Wanachana na mashabiki wa Simba, pamoja wa wadau wote wa soka, wakae mkao wa kula. Desemba 15, mwaka huu tunakwenda kushtua nchi, kwa sababu tutamtangaza mchezaji mkubwa tu kwenye ukanda huu," alisema Manara.

Hata hivyo Manara hakuwa tayari kutaja jina la mchezaji au wachezaji ambao itawasajili kwenye kikosi chao ambacho kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara kiko kwenye nafasi ya tatu, nyuma ya vinara Azam FC na Yanga.

Tetesi au uvumi huo unakuja kutokana na tetesi zingine kuwa Simba inakaribia kuachana na kiungo wake mkabaji raia wa Brazil, Gerson Fraga, ambaye amepata majeruhi yatakayomweka nje msimu mzima.

Naye Mkurugenzi wa Uwekezaji wa GSM ambao ni wadhamini wa Yanga, Hersi Said amewatoa wasiwasi wanachama na mashabiki wa klabu hiyo kuwa mchezaji huyo bado ni mali yao na ana mkataba wa miaka miwili.

Hersi alisema kwenye mkabata wowote duniani ni lazima kuwe na vipengele ambavyo vinatakiwa kutekelezwa na pande zote mbili, lakini kwa wao kila kitu kimetekelezwa.

"Ana mkataba wa miaka miwili na klabu ya Yanga, na tumelipa pesa zote za mkataba kwenye klabu ya AS Vita, tumelipa pesa yote ya uhamisho, hadai mshahara, anadai wa mwezi huu na ukiisha atalipwa, lakini pia ana furaha kwenye kikosi, kwa hiyo haya yote yanayoenezwa ni propaganda ambayo haiwezi kututoa katika azma yetu ya kuwa mabingwa msimu huu," alisema Hersi.

Yanga imekuwa mkali kuhusu Mukoko baada ya hivi karibuni kuzidiwa 'kete' na watani zao kwenye vita ya kumbakisha klabuni kiungo mshambuliaji, Bernard Morrison.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >